# Nipashe

Jumatano Desemba 6, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581516

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital | epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com




UKURASA 22

**ARTETA ATAKA RAMSDALE ABAKI**

MAAFA MANYARA

# Chanzo hiki hapa

• **Ripoti** ya wataalamu wa jiolojia yaanika kiini cha maporomoko ya tope... *Endelea ukurasa 2*




Operesheni ya kuyanasua magari yaliyokwama kwenye matope ikiendelea katika Mji Mdogo wa Katesh, wilayani Hanang', Manyara jana. **PICHA: GIFT THADEY**



UKURASA WA 4

**Rais** apitisha, Bima ya Afya kwa Wote sasa sheria rasmi

UKURASA WA 5

**Mhasibu** wa CWT adaiwa kujinyonga chooni ofisini

UKURASA WA 17

**Talaka** chanzo wanawake kupata ugonjwa wa akili




UKURASA WA 19

**Israel** kusababisha mafuriko Gaza



## Moto wateketeza maduka 32 jirani stendi ya Mwenge

UKURASA 4



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, wakimalizia kuzima moto uliyoteketeza maduka 32, eneo la Mwenge, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam usiku wa kuamkia jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Mvutano umri wa kuolewa wawagawa viongozi wa dini

UKURASA 5



Shehe Othman Zuberi Rebeca Gyumi Mch. Canon Matonya

**MICHEZO** RAYVANNY ANOGESHA VUNA DEILE YA ITV UK.20 **KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Wananchi wakiangalia mabaki ya gari dogo la abiria aina ya Toyota Hiace lenye namba za usajili T339 DBV, baada ya kupata ajali katika eneo la Kyetema, Kata ya Kyetema, wilayani Bukoba, mkoani Kagera jana na kusababisha vifo vya watu wanne na 21 kujeruhiwa. **Habari Uk. 3.** **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Chanzo maafa Manyara hiki hapa

**Na Waandishi Wetu**

KADRI uokoaji unavyoendelea, sambamba na miili ya waliofariki dunia kuzidi kuongezeka, ripoti ya awali kutoka kwa timu maalum ya wanajiolojia imebaini sababu ni Mlima Hanang', mkoani Manyara 'kushiba' maji, ukaelemewa.

Vilevile, wataalamu hao wamebaini mlima huo una chembe za volcano, jambo ambalo kitaalamu limechochea kuibuka kwa maporomoko hayo.

Jana Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, alifafanua kwamba miili iliyoongezeka hadi alasiri, ilikuwa mitatu, hivyo kufanya jumla yao 65. Kati yake, 60 ilikuwa imetambuliwa.

Aidha, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Gendabi kilichoathiriwa zaidi na maporomoko hayo, Damiano Yayeda, alisema wakazi wake 14 walikuwa hawajulikani walikokuwa hadi jana jioni.

Kwa mujibu wa Msemaji Mkuu wa Serikali, Matinyi, hadi jana, kaya 1,150 zilikuwa zimepoteza makazi yake kutokana na maafa hayo.

**RIPOTI YA UCHUNGUZI**

Matinyi alifafanua maudhui ya ripoti hiyo kutoka timu ya wataalamu wa Wizara ya Madini, kwamba chanzo cha maporomoko hayo yaliyoanzia kwa kumeguka Mlima Hanang', ni kutokana na mlima huo kunyonya maji mengi.

"Kimsingi, mlima huo una mi-amba dhoofu iliyonyonya maji mengi," alisema Matinyi huku akitaja hatua ya serikali kurejesha huduma za kijamii ikiwamo umeme.

**'TUSAIDIENI'**

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, jana aliyaalika mashirika ya misaada ya kimataifa, wafanyabiashara na taasisi mbalimbali nchini kupeleka misaada ya kibinadamu katika Wilaya ya Hanang' kuwasaidia waathirika wa maporomoko ya mawe, tope na maji walionusurika katika maafa hayo.

Akizungumza na wananchi wa Hanang' katika Mji wa Katesh, Waziri Mkuu Majaliwa alionya wanaofikiri wanaweza kunufaika na misaada hiyo akisema, "kusitokee makundi yatakayobeba dhamana ya kupokea misaada na ikawa fursa kwao.

"Hatutasita kuwachukulia hatua watakaohujumu misaada itakayotolewa. Tayari Ofisi ya Waziri Mkuu imepokea simu kutoka Mbeya, ambako yuko Mtanzania ameahidi kutoa katapila za kuondoa tope."

Waziri Mkuu alisema jopo la wataalamu linaendelea kufanya tathmini ya athari zilizotokea na serikali itatoa taarifa kuhusu jambo hilo.

Alisema serikali imeamua na imeelekeza miili iliyotambuliwa na kuagwa, isindikizwe na maofisa wake na vyombo vya usalama mpaka nyumbani kwa wafiwa.

"Mpaka jioni miili yote itakuwa imechukuliwa na ndani ya siku mbili mpaka tatu tunataka eneo hili liwe limekaa vizuri," alielekeza.

Waziri Mkuu pia alimwagiza Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Uratibu na Bunge, Jenista Mhagama, kukutana na mawaziri wenzake, wapange namna bora ya kuendelea na uokoaji na kurejesha hali ya Mji wa Katesh kwenye usafi.

Pia alielekeza wakuu wa mikoa ya Arusha, Dodoma na Singida kushirikiana na Mkuu wa Mkoa wa Manyara kuona namna ya kufanya kazi pamoja kutatua changamoto zilizojitokeza.

**MIILI 60 YATAMBULIWA**

Msemaji Mkuu wa Serikali, Matinyi, alisema hadi kufikia jana mchana, miili 60 ya watu waliopoteza maisha katika maafa hayo ilikuwa imetambuliwa na kuchukuliwa na ndugu zao, huku miili mitano ikiwa haijatambuliwa.

"Mkemia Mkuu wa Serikali ameelekezwa kuifanyia uchunguzi miili ambayo haijatambuliwa ili kubaini ndugu zao," alisema Matinyi.

**DK. SHOO**

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, alisema jana kuwa kanisa linaridhishwa na juhudi za serikali kuelekeza nguvu kubwa kwenye shughuli za uokoaji watu walionasa kwenye tope lililoporomoka kutoka Mlima Hanang' na kusababisha vifo na kujeruhi zaidi ya watu 110.

Akizungumza jana katika Kanisa Kuu la Usharika wa Moshi Mjini wakati wa ibada maalum ya kuaga mwili wa Askofu mstaafu wa Dayosisi ya Kaskazini, Dk. Erasto Kweka (89), Dk. Shoo, alisema kanisa linatambua kazi kubwa ambayo serikali inaendelea kuifanya katika Wilaya ya Hanang' kusaidia wananchi waliokumbwa na maafa ya maporomoko ya mawe, tope na maji.

"Nitoe pole nyingi kwa maafa yaliyotokea Hanang' tunaishukuru serikali, kwani toka yametokea maafa hayo, tumeona mmekimbilia kule na kuwekeza nguvu kubwa katika kuokoa na kuwasaidia wale waliopata maafa hayo.

"Pamoja na hilo, bado serikali imeona umuhimu wa kukutuma (Naibu Waziri Mkuu, Dk. Dotto Biteko) kuja kushirikiana nasi kumuaga baba yetu Dk. (Erasto) Kweka," alisema.

**SALAMA ZA MUFTI**

Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) limetoa salamu za pole kwa Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na maafa hayo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Katibu Mkuu wa BAKWATA, Alhaj Nuhu Mruma, Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Dk. Abubakar Zubeir, akiwa safarini Morocco, amepokea kwa masikitiko taarifa ya maafa hayo.

"Mufti Mkuu anatuma salamu za pole kwa Mheshimiwa Rais Samia, kwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara na kwa familia za ndugu zetu kutokana na janga hilo.

"Mwenyezi Mungu Mtukufu awape ndugu zetu wa Hanang' na wananchi wote wa Tanzania moyo wa subira kutokana na athari mbaya za janga hili," alisema.

***Imeandaliwa na Jaliwason Jasson (HANANG'), Godfrey Mushi (ARUSHA) na Romana Mallya (DAR)**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 05/12/2023

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe 06-12-2023 kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea DODOMA**, gari hilo lenye namba za usajili: **T 176 DFN / T 171 DFN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **18.00** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.80** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.00** |

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM hadi DODOMA kupitia MOROGORO ROAD.** Gari itasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

# Ajali, kipindupindu vyasababisha vifo

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WATU wanne wamefariki dunia na wengine 21 kujeruhiwa baada gari la abiria aina ya Haice lenye namba za usajili T 339 DVB lililokuwa linatoka Isimbya wilayani Bukoba kuelekea mjini Bukoba kupata ajali.

Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Kamishna Msaidizi Brasius Chatanda, ajali hiyo ilitokea jana saa 5:30 asubuhi eneo la Kyetema, Kata ya Kyetema.

Alibainisha kuwa watu watatu kati ya wanne waliofariki dunia ni watu wazima. Majeruhi ni watoto wanne na watu wazima ni 17 ambao walikuwa wanaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa.

Kamanda Chatanda alisema chanzo cha ajali ni mwendo kasi. Uchunguzi umebaini kuwa wakati akianza kuteremka, gari lilikuwa limewekwa huru (free) ilhali dereva alitambua eneo hilo lina mteremko mkali.

"Dereva alijaribu kurudi nyuma, gari likamshinda kwani mwendo aliokuwa nao ulikuwa ni mkali, hali iliyofanya ashindwe kulimudu," alisema kamanmda huyo na kubainisha kuwa karibu na eneo ambako ajali ilitokea, kuna maegesho ya bodaboda ambao pia aliwagonga lakini hakuna aliyefariki dunia.

**KIPINDUPINDU**

Katika hatua nyingine, ugonjwa wa kipindupindu umeukumba Mkoa wa Kagera, watu wanne wamefariki dunia huku wengine wanne wakiwa mahututi tangu ulipogundulika Novemba 29.

Taarifa ya mlipuko wa ugonjwa huo ilitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa Kagera, Fatma Mwassa katika mkutano na waandishi wa habari huku akiwataka wananchi kuendelea kuchukua taadhari hasa kipindi hiki cha mvua.

Alisema ugonjwa umelipuka katika Kijiji cha Buchurago, Kata ya Bugorora wilayani Missenyi. Kati ya watu wanne waliofariki dunia, watatu ni wa familia moja na wakazi wa wilayani Missenyi.

Mwassa alisema watu hao ni Mke na Mume pamoja na mama wa mume huku wengine ambao wanne ambao wako mahututi nao wakitokea wilaya hiyohiyo na wamelazwa katika Hospitali ya St. Teleza wakiendelea na matibabu.

Alibainisha kuwa watatu watatu walibainika kuwa na ugonjwa huo, lakini tayari wamepatiwa matibabu na kuruhusiwa kutoka hospitalini, akiwataka wananchi kuchukua tahadhari kutokana na ugonjwa huo kusambaa kwa haraka.



Askofu wa Kanisa la Mlima wa Moto, Rose Mgetta akizungumza na waandishi wa habari katika kanisa hilo, Mikocheni Dar es Salaam jana, kuhusu tamasha la SHILO linalotarajiwa kuzinduliwa siku ya Jumapili ijayo. Wengine ni waumini wa kanisa hilo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**


TEF Consult
Our business is to elevate your business

P.O. Box 33542, 23rd Floor,
Millenium Tower, Makumbusho,
Mob: +255 758 895 188
www.tef.co.tz
Email: info@tef.co.tz
5 December 2023

TANZANIA EMPOWERMENT FORUM

TAARIFA KWA UMMA



177424

**Hamphrey Shabani Abdallah**

Tunawasilisha kuomba usaidizi wa kumpata mwenye picha hapo juu, aliyetoweka tarehe 23 Machi 2023, akiwa na fedha za kampuni na hapatikani kwa nambari zake zote za simu.

Tafadhali fahamu kuwa mhusika hana mamlaka yoyote ya kuwakilisha, kuendesha biashara yoyote, au kufanya kazi kwa wadhifa wowote kwa niaba ya Tanzania Empowerment Forum Limited au Airtel, ambaye alishirikiana naye hapo awali. Ni muhimu kutambua kwamba kampuni haitawajibika kwa mikataba yoyote, miamala au taarifa zitakazotolewa naye kwa niaba ya kampuni..

Tafadhali wasiliana nasi kwa +255 (0) 758 895 188 kama una taarifa yoyote kuhusu Hamphrey au unajua mahali alipo.

Uongozi
Tanzania Empowerment Forum


# MSD yasambaza vifaa tiba vya milioni 930/- Ulanga

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Bohari ya Dawa (MSD), Kanda ya Dar es Salaam imesambaza vifaa tiba vya zaidi ya Sh. milioni 930 kwa ajili ya vituo vya afya 23 vya Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga.

Mbunge wa Ulanga, Salim Hasham alisema, wamepokea vifaa tiba hivyo na dawa za zaidi ya Sh. milioni 900 kwa ajili ya vituo vya afya 23 vya halmashauri hiyo.

Alisema hatua ya kupokea vifaa hivyo vya kisasa ni mwendelezo wa maboresho sekta ya afya, Ulanga na Mkoa wa Morogoro.

"Huu ni utekelezaji wa Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi ibara ya 83 sura ya 3 na kwa kiasi kikubwa Mwenyekiti wetu wa Chama ambaye ndiye Rais anatutendea haki sisi wanachama kwa kufanya zaidi ya matarajio yetu, sekta ya afya ni muhimu kwa maendeleo ya taifa hili.

"Tunaona mabadiliko kwa bohari yetu ya dawa ni makubwa sana kwa miaka mitatu ya hivi karibuni, hapa kwetu Hospitali ya wilaya ilikuwa na shida ya X-Ray kwa zaidi ya miaka minne, lakini tumepata na watu waliokuwa wakienda kupata huduma wilaya nyingine sasa hawahangaiki tena," alisema.

Alisema, pia wamepokea Sh. milioni 900 kwa ajili ya ukarabati wa hospitali ya wilaya hiyo na mazungumzo yanaendelea ili waweze kupatiwa eneo lingine litakalokidhi mahitaji ya wilaya hiyo ambayo kwa sasa ni makubwa yakihusisha wawekezaji na wafanyabiashara wa madini ambao watapatiwa huduma.

"Zamani vituo vya afya vilikuwa vinaisha na tunakaa kusubiri vifaatiba zaidi ya mwaka, lakini kwa sasa vinasubiri mmalize wafunge na wananchi wapate huduma kwa wakati mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, MSD mabadiliko ni makubwa sana," alisisitiza.

Meneja wa MSD Kanda ya Dar es Salaam, Betie Kaema alisema, kwa niaba ya serikali wanaahidi kutomwangusha Rais katika utekelezaji wa majukumu yake, upatikanaji wa uhakika wa dawa na vifaa tiba nchini utaendelea kuimarika zaidi kuboresha huduma za afya.

"Julai hadi Novemba tumehakikisha dawa na vifaa tiba vya Sh. milioni 600 vinaletwa hapa na sasa tumekabidhi dawa na vifaa tiba vya zaidi ya Sh. milioni 300, vituo vya afya 23 vya Ulanga watapata bidhaa za Sh. milioni 900 ambazo zote zimekamilika na sasa vinasambazwa vituoni.

Alitaja baadhi ya vifaa tiba ambavyo wamepatiwa wananchi wa Ulanga ni pamoja na kiti cha huduma ya meno, vitanda vya huduma ya uchunguzi, vitanda vya wodini vya wagonjwa, vifaa vya joto kwa ajili ya watoto njiti, vifaa vya kusaidia upumuaji, vifaa vya oxygen, vitanda vya upasuaji na mashine ya Ultrasound.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ulanga, Alli Ramadhan, alisema kwa sasa hali ya huduma za afya wilayani humo imekuwa na maboresho makubwa kuanzia watumishi, dawa na vifaa tiba.


KILIMANJARO DRINKING WATER
A PRODUCT OF The Coca-Cola Company




Mshindi wa
SUPERBRANDS AFRIKA MASHARIKI 2022-2024

VOTED Superbrands EAST AFRICA'S CHOICE 2022-2024

Asanteni wateja wetu
Hii ni yetu sote

kilimanjaro_drinking_water | kilimanjarodrinkingwater | kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

# Rais atia saini Muswada Bima ya Afya kwa wote

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HATIMAYE Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Na. 8 wa Mwaka 2022, umetiwa saini na Rais Samia Suluhu Hassan na sasa umekuwa sheria kamili baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Desemba Mosi, mwaka huu.

Mwezi uliopita, Bunge lilipitisha muswada huo ambao pamoja na mambo mengine, umeainisha vyanzo tisa vya mapato vitakavyotumika kupata fedha za kuhudumia Bima ya Afya kwa Wote.

Baada ya kutiwa saini sheria hiyo, hatua inayofuata ni utungaji kanuni kwa ajili ya kuanza utekelezaji na jukumu litafanywa na Wizara ya Afya.

Kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Instagram, Waziri wa Afya Ummy Mwalimu alithibitisha kutiwa saini muswada huo, akisema "Alhamdulilah! Shukrani sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kujali afya za wananchi wako hususan wa kipato cha chini.

"Kazi iliyo mbele yetu sasa ni kuhakikisha utekelezaji wa sheria hii kwa ufanisi na kwa manufaa ya Watanzania hususan wa kipato cha chini ili kuwawezesha kupata huduma bora za afya bila ya kikwazo cha fedha."

Waziri Ummy, akiwasilisha bungeni muswada huo, alivitaja vyanzo vinajumuisha mapato yatokanayo na ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vyenye kaboni, vinywaji vikali, bidhaa za vipodozi, kodi ya michezo ya kubahatisha, ada ya bima za vyombo vya moto.

Alitaja vyanzo vingine ni mapato yatokanayo na ushuru wa miamala ya kielektroniki kwa kadri itakavyopendekezwa na waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha, fedha zitakazotengwa na Bunge, mapato yatokanayo na uwekezaji wa mfuko na zawadi na misaada kutoka kwa wadau mbalimbali.

Waziri huyo alisema kifungu cha saba cha sheria hiyo kinaainisha majukumu ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) katika kudhibiti na kusimamia mfumo wa bima ya afya nchini.

Alisema kwa mujibu wa kifungu hicho, TIRA pamoja na mambo mengine, itakuwa na wajibu wa kusajili na kudhibiti skimu za bima ya afya, kuhakikisha kuwa kila skimu ya bima ya afya inatoa kitita cha mafao ya huduma muhimu kwa mujibu wa sheria hiyo.

Alisema wajibu mwingine wa TIRA ni kutoa miongozo kuhusiana na uendeshaji wenye tija na ufanisi wa shughuli za skimu za bima ya afya.

Waziri Ummy pia alisema katika kufikia lengo la Bima ya Afya kwa Wote na kwa kutambua uzoefu na uwekezaji uliofanywa na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF), serikali inapendekeza kufanya marekebisho kwa kuanzisha kitita cha Bima ya Afya cha Jamii (CHIP) ikiwa ni mpango mbadala wa CHF ambao sheria iliyoanzisha mfuko huo inapendekezwa kufutwa na kuianzisha upya chini ya sheria hiyo.

"Lengo la kuanzishwa kwa kitita hicho ni kuhakikisha wananchi wote wanajumuishwa katika utaratibu wa bima ya afya ili kupata huduma bora za afya pasi na vikwazo wanavyokutana navyo sasa," alisema Ummy.

Alivitaja vikwazo hivyo ni wananchi kutopata huduma za afya wanapokuwa nje ya maeneo waliyojiandikisha na hivyo kulazimika kulipia huduma za afya kwa utaratibu wa papo kwa papo, hali inayoathiri shughuli za kijamii na kiuchumi.

Kikwazo kingine ni wigo mdogo wa kuchangiana kati ya mikoa na halmashauri zenye uchumi mkubwa na mdogo, wananchi wenye kipato kikubwa na kidogo na wagonjwa na wasio wagonjwa kutokana na kusimamiwa katika ngazi za mamlaka za serikali za mitaa.



Alitaja kikwazo kingine ni ufinyu wa huduma katika kitita cha mafao kinachotolewa, hivyo kukosekana huduma muhimu, mathalani huduma za afya ya kinywa na meno, kutojumuishwa kwa baadhi ya dawa na hivyo kumlazimu mwanachama kulipia.

Kikwazo kingine ni muundo wa CHF kutokidhi misingi na kanuni za uendeshaji bima ya afya, mathalani kutotenganisha kwa majukumu kati ya mnunuzi na mtoa huduma za afya.

Alitaja kikwazo kingine ni uhiari wa wananchi kujiunga unaosababisha wananchi kujiunga wakiwa wagonjwa.

Waziri Ummy alisema kifungu cha 21 cha sheria hiyo kinaweka viwango vya uchangiaji kwa wanachama kutoka sekta ya umma, sekta rasmi binafsi na sekta isiyo rasmi.

Alisema serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu hicho kwa kubainisha kuwa mchango wa asilimia sita wa mshahara utakuwa kwa ajili ya mwajiri wa sekta ya umma na mwajiri wa sekta rasmi binafsi atakayechagua kuwasajili waajiriwa wake katika skimu ya bima ya afya ya umma.

"Kwa muktadha wa sheria hii, mshahara wa sekta ya umma na sekta rasmi binafsi umetafsiriwa kwa maana sawa na ile inayotumika na mifuko ya hifadhi ya jamii kwa sekta zote mbili mtawalia.

"Dhumuni la kifungu hiki ni kuwa na maana zinazofanana na kuhakikisha kuwapo uwiano katika uchangiaji wa kitita cha mafao ya huduma muhimu," alisema.

Waziri Ummy alisema kifungu cha 25 kinaweka masharti kuhusiana na ukomo wa uanachama ambapo uanachama utafikia ukomo iwapo mwanachama atafariki dunia au ataacha kuchangia katika skimu ya bima ya afya.

Alisema kifungu kinabainisha kuwa wategemezi wa mwanachama aliyefariki dunia, wataendelea kupata huduma kwa kipindi kitakachobainishwa na waziri mwenye dhamana katika kanuni.

Waziri Ummy alisema dhumuni la kifungu hicho ni kulinda haki za wategemezi wa mwanachama.

Alisema sehemu ya sita inaweka masharti kuhusu udhibiti ubora wa huduma zitolewazo na vituo vya kutolea huduma za afya na skimu za bima ya afya.

Alisema kifungu cha 26 kina lengo la kuhakikisha skimu za bima ya afya zinazingatia ubora katika utoaji huduma za bima ya afya kulingana na miongozo ya TIRA.

Alisema kifungu cha 27 kinaipa Wizara ya Afya jukumu la kuhakikisha vituo vya kutolea huduma za afya vilivyoingia mikataba na skimu za bima ya afya za umma na binafsi vinatoa huduma bora za afya kwa wanufaika kwa kuzingatia viwango vya ubora vilivyotolewa na wizara.

Waziri Ummy alisema kifungu cha 34 cha sheria hiyo kinaweka katazo kwa wanufaika, vituo vya kutolea huduma za afya na skimu za bima ya afya na mtu yeyote kutoa taarifa za uongo na kuweka adhabu iwapo watathibitika kufanya hivyo.

Alisema dhumuni la kifungu hicho ni kulinda uhai na uendelevu wa skimu za bima ya afya kwa kuzuia masuala ya udanganyifu na ubadhirifu wa fedha za wanachama ili kuhakikisha huduma za bima ya afya zinazotolewa zinakidhi vigezo na ni endelevu.

Waziri Ummy alisema serikali inapendekeza kufanya marekebisho kwa kuweka adhabu ya asilimia 10 ya mchango wa kila mwaka kwa mtu yeyote ambaye hatajiunga na bima ya afya kwa kipindi cha miaka mitatu tangu kuanza kutekelezwa kwa sheria inayopendekezwa.

Alisema waziri amepewa mamlaka ya kutoa msamaha wa ulipaji wa adhabu ya asilimia 10 kwa kuzingatia maslahi ya umma au sababu nyingine yoyote.

## Moto wateketeza maduka 32 Mwenge

**Na Romana Mallya**

MADUKA 32 ya wafanyabiashara, yameteketea kwa moto uliozuka usiku wa kuamkia jana eneo la stendi ya Mwenge, wilayani Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Baadhi ya wafanyabiashara hao wamepoteza fedha walizokuwa wamehifadhi kwenye maduka hayo.

Tukio hilo limetokea huku ikiwa takribani miezi miwili tangu maduka, vibanda vya wafanyabiashara Soko la Mnadani, Kariakoo, kuteketea kwa moto Oktoba Mosi, mwaka huu.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, akizungumza jana eneo la tukio, aliuagiza uongozi wa Halmashauri ya Kinondoni kukaa na wafanyabiashara hao ili kuangalia njia ya haraka ya kuwasaidia.

"Kama kuna fedha mahali wakopeshwe ili warudi katika mfumo angalau kwa riba ndogo ndogo, tufanye hivyo kwa haraka. Tunasema si kuwapa bure, kama kuna akiba mahali fulani kwa kuanzia, kwa sababu hawa wanafamilia na moto huu hawajauchoma wao.

"Lakini baada ya vyombo kujua watakuja kutuambia nani hasa amesababisha, ninajua kuna bahati mbaya na kuna kitu kinachoitwa tukio la kupangwa, haya hatuwezi kuyathibitisha leo ni mpaka timu au kamati ndogo iundwe na Mkuu wa wilaya baada ya hapo vyombo vya usalama vitatuongoza nini cha kufanya," alisema.

Chalamila alisema amejaribu kuwauliza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) pamoja na kikosi cha Zimamoto nini chanzo cha moto huo, wote wameomba wapewe muda kufuatilia.

"Nimewauliza watu wa TANESCO kama ni hitilafu ya umeme wamesema 'tupe muda kidogo', nimewauliza watu wa Fire (Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji) wamesema 'tupe muda kidogo'.

"Kwa ujumla hasara iliyopatikana hapa aihitaji kwenda chuo kikuu kujifunza na kwa bahati mbaya sana imeonesha wafanyabiashara wengi hawajui thamani ya benki kwa sababu ndani ya moto huu kuna fedha nyingi ambazo zimeungua," alisema.

Chalamila alisema katika eneo la tukio kuna vipande vingi vya Sh. 10,000 ambavyo vimezagaa vikiwa vimeungua.

Alisema kuna haja ya kujipa miezi sita ya kuboresha maeneo hayo ambayo yanahitaji ujenzi unaoweza kuzuia moto.

"Jambo la pili ni kuangalia majengo ili kama kuna jengo moja limepata moto, lingine lisipate madhara, kuangalia pia, vifaa vinavyoweza kuzuia moto ili matukio kama haya yafikie mwisho," alisema.

Pia, alisema elimu nyingine inayohitajika ni ya bima kwa wamiliki wa jengo ili tatizo linapotokea watu waweze kufidiwa, kwa kuwa kinyume na hapo huwa ni hasara.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambale, alisema tayari timu ya uchunguzi imeundwa inayohusisha TANESCO, Kikosi cha Zimamoto na wataalam wa ardhi ili kubaini chanzo cha moto huo.

Mfanyabiashara sokoni hapo alisema tatizo hilo limewaumiza na kuomba uongozi uwaeleze chanzo chake ni nini na watafidiwaje.

Mfanyabiashara mwingine wa duka la nguo, Lilian alisema hakuna alichoweza kuokoa ndani ya duka lake.

Mlinzi wa eneo hilo, Gadiola alisema wakati tukio hilo linaanza saa sita kamili usiku alikuwapo lakini pamoja na kutoa taarifa kwa kikosi cha zimamoto, kilichelewa kufika.

"Moto ulianza kwenye jengo la kwanza ukasogea mpaka kwenye jengo la pili la mwisho, tulijaribu kuuzima tukashindwa ulikuwa mkubwa.

"Chanzo cha moto nilivyoona ni shoti ya umeme ilipiga kwenye chumba cha kwanza, umeme haukukatika na kurudi, ila siku za nyuma ulikuwa na tabia ya kukatika na kurudi," alisema.

Alisema baadhi ya wafanyabiashara usiku ule walipigiwa simu, lakini licha ya kurudi hawakufanikiwa kuokoa mali zao.

Mwaka 2015, tukio la moto liliwahi kutokea katika soko la Mwenge na kuteketeza maduka kadhaa, lakini ulidhibitiwa na Kikosi cha Zimamoto.

# Mhasibu wa CWT adaiwa kujinyonga choo cha ofisini

**Na Hamisi Nasri,**
MASASI

MHASIBU wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara ambaye ni Mratibu Elimu Kata, Kata ya Matawale, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Angelus Mwinyuku (46) amefariki dunia, akidaiwa kujinyonga katika choo cha ofisi ya chama hicho kwa kutumia kamba ya manila. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Kamishna Msaidizi Nikodemus Katembo, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea juzi saa 12 jioni wilayani Masasi katika ofisi ya CWT iliyoko Mtaa wa Wapiwapi, Kata ya Nyasa.

Alieleza kuwa mwili wa mhasibu huyo ulikutwa chooni ukining'inia kwenye kamba hiyo ya manila iliyofungwa katika dirisha.

Alisema kuwa baada ya Jeshi la Polisi kupata taarifa za tukio hilo, lilifika katika eneo la tukio kwa ajili ya kushuhudia na kufanya uchunguzi wa tukio hilo.

Kamanda Katembo alisema sababu za mhasibu huyo kujinyonga bado hazijajulikana. Uchunguzi zaidi unaendelea kufanywa na jeshi hilo.

Alisema Jeshi la Polisi litatoa taarifa kuhusu chanzo cha kifo cha mhasibu huyo baada ya kukamilisha uchunguzi.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mji Masasi, Salumu Gembe alithibitisha kupokea mwili wa mhasibu huyo juzi saa moja usiku na kuuhifadhi katika chumba cha kuhifadhi maiti cha hospitali hiyo.

Mwenyekiti wa CWT Wilaya ya Masasi, Thabiti Thabiti, alisema chama hicho kimepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo hicho. Kinatoa pole kwa ndugu na jamaa wa mhasibu huyo.

# Mvutano umri wa kuolewa wawagawa viongozi wa dini

**Na Waandishi Wetu**

VIFUNGU namba 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 vinavyoruhusu mtoto kuoa na kuolewa akiwa na umri wa miaka 14 na 15, bado ni kizungumkuti. Viongozi wa dini wametofautiana kwa mara nyingine kuhusu umri sahihi wa mtoto kuolewa.

Baadhi wamependekeza vifungu hivyo virekebishwe na kutamka umri wa chini kuolewa uanzie miaka 18 huku wengine wakitaka uamuzi wa umri ubakie kwa wazazi wa binti na viongozi wa dini wanaofungisha ndoa.

Utofauti huo wa maoni ulitokea jana jijini Dar es Salaam wakati wa kongamano la viongozi wa dini na wadau wengine kuhusu umri halali wa ndoa, uliowakutanisha viongozi wa dini za Kikristo, Kiislamu, wanaharakati, wanasheria na wasaidizi wa kisheria kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Katika mjadala huo, Mwanaharakati Rebeca Gyumi alisema ni muhimu kuwa na sheria inayomtafsiri mtoto katika uhalisia bila kujali kama yuko shuleni au nje ya mfumo wa elimu, ili kuzuia ndoa za utotoni.

"Kwa sasa kuna mkanganyiko na ndio maana tunatamani Sheria ya Ndoa irekebishwe kwa sababu mtu akimwoa mtoto mwenye umri chini ya miaka 18 au zaidi ambaye ni mwanafunzi, anakabiliwa na hatia kwa mujibu wa Sheria ya Elimu, lakini akiolewa binti wa miaka 14 ambaye yuko nje ya mfumo wa elimu inakuwa ni tabu kubwa.

"Inasikitisha kwamba mtu aliye chini ya miaka 18 haruhusiwi kuingia mkataba, kupiga kura wala kupewa leseni ya udereva, lakini mtoto huyo huyo aonekane anaweza kubeba jukumu la ndoa na familia," alisema.

Aliongeza kuwa mwanya wa kifungu cha 13 na 17, kuruhusu binti aolewe akiwa na miaka 14, kinawaumiza zaidi watoto wa maskini wanaokabiliwa na changamoto za maisha duni yanayochangia washindwe kuendelea na shule.

Alisema watoto wengi wanaokumbwa na ndoa za utotoni, wanalazimishwa na baadhi wanaelekezwa kufeli mitihani ili wasiendelee na shule na waolewe.

Alitoa mfano kuwa katika miaka ya hivi karibuni, nchi za Malawi, Bangladesh, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na Zimbabwe zimeidhinisha kuwa umri wa kuoa na kuolewa si chini ya miaka 18.

Mkurugenzi wa Kurugenzi wa Kichungaji wa Baraza la Maaskofu Katoliki (TEC), Padre Florence Rutaihwa, alisema sheria ya kanisa hilo kifungu cha 1071 inalitaka kanisa kuruhusu ndoa isiyokinzana na sheria za nchi.

"Kwahiyo, sisi tunakubali umri wa mtoto uanzie miaka 18," alisema.

Katibu wa Taifa wa Jumuiya ya Vijana wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Sheikh Othman Zuberi, alisema Uislamu ni dini inayozingatia maslahi na kwamba Quran haijaweka umri wa mtoto kuoa au kuolewa ili wazazi wapime maslahi ya kuruhusu au kupinga.

"Tusimtetee tu mtoto wa kike ambaye utandawazi umemfanya ajue kila kitu... tumeona watoto wa darasa la tatu, la nne wanapewa vidonge vya kuzuia ujauzito, maana yake ni kwamba mtoto huyo ameshajiingiza kwenye uhusiano wa kimapenzi," alisema.

Kiongozi huyo wa kiroho alisema hawezi kuruhusu mtoto wake aolewe akiwa na miaka 18 kwa kuwa analinda maslahi yake ya elimu.

"Nina watoto wanane na mmoja yuko kidato cha tano, mwingine amemaliza kidato cha nne, siko tayari kumwozesha kwa sasa," alisisitiza.

Sheikh Maulidi Kidebe wa Wilaya ya Ubungo, alitaka umri wa kuolewa usitamkwe kisheria na badala yake uamuliwe na wazazi wa binti.

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Mch. Canon Matonya, alisema umoja huo unaunga mkono umri wa ndoa uanzie miaka 18 na kwamba kuruhusu aolewe kabla ya hapo ni kumnyima haki zake za msingi.

"Mtoto akiolewa katika umri mdogo, anakosa fursa nyingi sana za kustawi. Akiolewa mapema anakosa fursa nyingi ambazo Mungu alimwekea kama za elimu, kiuongozi na kiafya," alisema.

Alikumbusha kuwa wataalamu wa afya wanakumbusha hatari ya kifo kwa mimba za utotoni kutokana na mwili wa mtoto kutokuwa tayari kimaumbile kubeba ujauzito.

Mkuu wa Dawati la Jinsia Kanda Maalum ya Dar es Salaam, ACP Leah Mbunda, alisema matukio mengi ya ukatili wa kijinsia yanatokea kwenye ndoa na walioolewa katika umri mdogo wanakabiliwa na unyanyasaji mkubwa zaidi.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inapenda kuwakumbusha viongozi wote wa umma walioainishwa kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Sura ya 398), kuwa upokeaji wa Tamko la Rasilimali, Maslahi na Madeni kwa mwaka 2023, umeanza tangu tarehe 01 Oktoba, 2023 na utamalizika tarehe 31 Desemba, 2023.

Uwasilishaji wa Tamko hilo kwa Kamishna wa Maadili ni kwa mujibu wa kifungu cha 9(1)(b) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kwamba kutoa Tamko la uongo, potofu, kuchelewa ama kushindwa kuwasilisha Tamko hilo kwa kipindi kilichoainishwa ni ukiukwaji wa maadili kwa mujibu wa kifungu cha 16 cha Sheria tajwa.

Kiongozi anatakiwa kupakua fomu katika tovuti ya Taasisi yenye anwani www.maadili.go.tz na kuijaza kisha kuwasilisha Tamko husika kwa kufika moja kwa moja katika Ofisi za Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Makao Makuu zilizoko Jengo la PSSSF Kambarage, Mtaa wa Jakaya Kikwete - Dodoma, Ofisi za Kanda ya Kati zilizoko Viwanja vya Nanenane – Dodoma, Ofisi za Kanda Maalum Dar es Salaam zilizoko Barabara ya Ohio karibu na Benki ya CRDB Holland House, Dar es Salaam, Ofisi za Kanda ya Kaskazini zilizoko katika Jengo la Hazina – Arusha, Ofisi za Kanda ya Ziwa zilizoko Jengo la NSSF, Mtaa wa Kenyatta - Mwanza, Ofisi za Kanda ya Nyanda za Juu Kusini zilizoko Jengo la NHIF – Mbeya, Ofisi za Kanda ya Mashariki zilizoko Jengo la NSSF – Morogoro, Ofisi za Kanda ya Magharibi zilizoko Mkabala na Hoteli ya Orion – Tabora na Ofisi za Kanda ya Kusini zilizoko Jengo la Maadili – Mtwara, Mtaa wa Chikongola Barabara ya TANU. Aidha, kiongozi anaweza pia kuwasilisha Tamko kwa njia ya posta kupitia "registered mail" ikiwemo "ems."

Viongozi wanakumbushwa kuwa Tamko linalopokelewa ni nakala halisi (Original Copy) na sio lililorudufiwa (Photocopy) au lililokuwa "scanned" na kutumwa kwa njia ya baruapepe.

*Imetolewa na:* **KAMISHNA WA MAADILI**
**SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**
**6 Desemba, 2023**

177439

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# COP28 matarajio ya Watanzania kuleta mabadiliko

**MKUTANO** wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) unawakutanisha wajumbe kutoka mataifa yapatayo 200 duniani, wakiwamo wakuu wa nchi, viongozi wa taasisi za kifedha na biashara, wawakilishi wa taasisi za serikali pamoja na asasi za kiraia.

Mkutano huo unafanyika Dubai tangu Novemba 30 na utahitimishwa Desemba 12, 2023.

Wajumbe wa mkutano huo wameridhia kuanzishwa kwa mfuko uliokuwa unangojewa kwa muda mrefu wa kulipa fidia ya madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi, yanayosababishwa na mvua zenye madhara na ukame.

Makubaliano kama hayo hufikiwa siku za mwisho wa mkutano baada ya siku kadhaa za majadiliano, lakini katika mkutano huo makubaliano hayo yamefikiwa katika siku ya kwanza ya COP28.

Katika kuitikia wito wa kuanzishwa kwa mkutano huo Umoja wa Ulaya, Uingereza na Marekani pamoja na mataifa mengine, walitangaza kuchangia Dola za Marekani milioni 400, kwa mataifa maskini yanayokabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Baada ya kuafikiwa kuanzishwa kwa Mfuko wa Kulipa Fidia ya Madhara ya Tabianchi, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) uliahidi kutoa Dola milioni 100, Ujerumani Dola milioni 100. Marekani ilisema itatoa dola milioni 17, iwapo itafikia makubaliano kwenye mkutano huo.

Ujumbe wa Tanzania COP28 unaoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan na kushirikisha mawaziri, makatibu wakuu, mabalozi, viongozi na wataalamu kutoka wizara za kisekta, idara za serikali, mashirika ya umma, vyuo vikuu, sekta binafsi, asasi za kiraia, vijana na wanahabari kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Katika hotuba yake Rais Samia ameyataka mataifa duniani kutambua kuwa suluhisho la uhakika la kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ni kutimiza ahadi za kutoa fedha na kuongeza kasi ya mikakati ya kukabiliana na janga hilo.

Katika hotuba yake Rais Samia alikumbusha kushindwa kutimiza ahadi kunapunguza mshikamano na imani na kuleta matokeo mabaya kwa nchi zinazoendelea, ikiwamo Tanzania, ambayo hupoteza kati ya asilimia mbili hadi tatu ya Pato la Taifa (GDP) kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Katika uzinduzi wa mradi wa nishati safi ya kupikia kwa wanawake Afrika (AWCCSP) inayokusudia kuleta mageuzi na kumkomboa mwanamke, Rais Samia Suluhu Hassan alitumia dakika 15 kuyashawishi mataifa ya Afrika kushiriki kikamilifu utekelezaji wa mradi huo.

Tukio hilo la uzinduzi wa mradi huo muhimu wa nishati safi ya kupikia kwa wanawake Afrika lilifanyika Desemba 2, ikiwa ni sehemu ya Mkutano wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabiachi (COP28) unaoendelea huko Dubai.

Washiriki wote walisimama huku wakitazama video iliyohesabu namba kutoka tisa hadi moja na kuonekana jiko la gesi lenye herufi za AWCCSP, ambazo ni ufupisho wa jina la mradi huo.

Rais Samia amezindua mradi huo wa AWCCSP ngazi ya Afrika, baada ya kuanza utekelezaji wa Dira ya miaka 10 inayokusudia kuongeza matumizi ya nishati safi za kupikia kwa asilimia 80 ya Watanzania wote.

Programu hiyo inalenga kuhamasisha matumzi ya nishati safi ya kupikia ili kukabiliana na changamoto za afya, mazingira, uchumi na kijamii ambazo huathiri zaidi wanawake na watoto, kutokana na ukweli kuwa hutumia muda mrefu kutafuta kuni, programu hiyo itawasaidia kupata muda wa kutosha kushiriki kwenye shughuli za maendeleo.

Matarajio ya Tanzania kwenye mkutano wa COP28 ni pamoja na kuhakikisha msimamo wa nchi unakubaliwa kwa kupata fursa za upatikanaji wa rasilimali fedha, kuwezesha miradi ya pamoja na teknolojia za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Golden Kisapile, TUDARCO.

# CCTV zinaweza kukomesha ukatili

**MAWIMBI** ya sakata la kiongozi wa serikali bado yanasambaa ni baada ya video kuingia mitandaoni , ikidaiwa anahusika na kumdhalilisha kijana aliyedaiwa kuwa anakwamisha biashara yake huko Babati mkoani Manyara.

Baada ya tukio hilo Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) ukajinasibu kuzunguka nchi nzima kupinga ukatili wa kijinsia na kuporomoka kwa maadili ,na kusema endapo tuhuma hizi zitathibitika hatua zitachukuliwa dhidi ya kiongozi mtuhumiwa.

Ukatili wa kijinsia ni ujumla wa vitendo vyenye nia ya kuwadhulumu, kuwanyanyasa, au kuwadhuru watu kwa kulenga jinsi yao na hufanyika popote kazini, shuleni, nyumbani, kazini na mitaani ndani ya jamii.

Nikiachana na udhalilishaji wa Babati , nizungumzie suala la kamera zinazorekodi matukio au 'CCTV cameras' hasa zilizofichwa au zisizoonekana kwa urahisi ambazo hutumiwa kurekodi matukio na shughuli zinazotokea katika eneo fulani.

Vifaa hivi vinaweza kuwa na umuhimu katika kuzuia na kukusanya ushahidi wa matukio ya ukatili wa kijinsia, kama unyanyasaji au udhalilishaji ili wahusika wachukuliwe hatua pia kudhibiti matukio hayo.

Uwepo wa kamera za siri unaweza kuwapa hofu wanaotaka kufanya ukatili hivyo kusita, wakihofia kurekodiwa. Kwa mfano, mwanafunzi au mwalimu yeyote shuleni anayewaza kufanya unyanyasaji anaweza kusita akiogopa kamera.

Kamera za siri zinaweza kutoa ushahidi muhimu katika kubaini na kuwafikisha mahakamani wahusika katika visa vya ukatili kwa mfano ubakaji, ulawiti, vipigo na kutesa wanafunzi katika bweni.

Kwa upande mwingine ni nyenzo ya kujua kuwa vitendo vyao vinachunguzwa , hayo yanawafanya wanafunzi na wafanyakazi kuwa na uwajibikaji zaidi na kujitahidi kuwa na tabia nzuri. Kwa mfano, wanafunzi wanaweza kuepuka kufanya ukatili au udhalilishaji kwa sababu wanajua watanaswa.

Majibu ya haraka na ufuatiliaji wa moja kwa moja wa taarifa za kamera za siri yanaruhusu hatua za haraka kuchukuliwa ikiwa kuna shaka au ukatili uliofanyika, kwa mfano, ikiwa kamera inaonyesha mkasa ukitokea, hatua za dharura zinaweza kuchukuliwa kuudhibiti mara moja.

Uhamasishaji na elimu ni jambo linaloweza kufanyika pia kwa kufunga kamera kwa vile zinaweza kuongeza uelewa, majadiliano juu ya kuzuia na kusaidia waathirika, kwa mfano, kamera zinaweza kutumiwa kama zana ya kuelimisha wanafunzi na wafanyakazi athari za kufanya uovu na kuuzuia.

Kadhalika, kamera za siri zinasaidia waathirika kwa kutoa ushahidi unaothibitisha madai yao na kutafuta haki. Kwa mfano, mwanafunzi anayepitia unyanyasaji anaweza kutumia rekodi za kamera kama ushahidi wa kufanikisha haki kwenye kesi yake.

Aidha, kuhakikisha wafanyakazi wanatekeleza wajibu wao wa kulinda wanafunzi, mali za shule na kuchukua hatua sahihi kwa visa vyovyote vya ukatili au uharibifu wowote. Kwa mfano, kamera zinaweza kusaidia kufuatilia tabia ya wafanyakazi na kubaini ikiwa kuna ukiukwaji wa maadili au vitendo vya ukatili.

Mambo hayaishi hapo pia zinawapa wazazi na walezi uhakika, wakijua kuwa watoto wao wanachunguzwa na kulindwa. Kwa mfano, wanaweza kuwa na amani wanapojua kuwa kuna kamera zinazofuatilia shughuli na mienendo mabwenini na kuzuia ukatili wa kijinsia na uhalifu.

Kuchambua rekodi na taarifa za kamera kunafanikisha kutambua mifumo ya ukatili, shule kutekeleza mikakati ya kuzuia inayolenga maeneo maalum. Kwa mfano, kwa kuchunguza rekodi za kamera, shule itagundua mwenendo wa ukatili na kuchukua hatua za kuzuia na kuadhibu watuhumiwa.

Hatimaye, uwepo wa kamera za siri huchangia katika kuunda mazingira salama na yenye usalama kwa wanafunzi , kupunguza hatari ya ukatili wa kijinsia. Kwa mfano, kamera zinasaidia kujenga utamaduni wa kuheshimiana na kuzuia vitendo vya ukatili katika mabweni na popote pale shuleni.

Hivyo iwapo serikali itaagiza kufungwa CCTV itakuwa imepunguza madhara ya kiafya, majeraha ya kimwili, kihisia na magonjwa kama ya ngono na mimba zisizotarajiwa. Lakini pia waathirika wa ukatili wa kijinsia wanaweza kukumbwa na msongo wa mawazo, wasiwasi, unyonge na hata matatizo ya akili.

Hata hivyo, ni muhimu kuzingatia kuwa kamera za CCTV zinapaswa kuambatana na mipango kamili ya kuzuia ukatili wa kijinsia, sera, na huduma za usaidizi ili kukabiliana na sababu za msingi za ukatili huo kwa Watanzania.

## NMB yang'ara tuzo za ATE

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imenyakua tuzo nne kwenye Tuzo za Mwajiri Bora wa Mwaka (EYA 2023), ukiwamo ushindi wa pili kwenye Mshindi wa Jumla wa tuzo hizo zilizotolewa jana jijini Dar es Salaam na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE).

Tuzo nyingine ilizoshinda benki hiyo ni za mshindi wa pili wa Sekta Binafsi, wa kwanza katika Ubora, Tija na Ubunifu, na wa kwanza pia kwenye Masuala ya Usawa wa Kijinsia.

Hii ni mara ya pili mfululizo kwa benki hiyo kung'ara kwenye tuzo hizo za kila mwaka baada ya kutangazwa kuwa Mwajiri Bora wa Mwaka 2022 na kushinda tuzo nyingine mbili kutokana na ubora wake wa kibiashara na katika usimamizi wa rasilimali watu.

Tangu mwaka 2005, ATE imezitumia tuzo hizi kuhamasisha na kutunuku mashirika yanayozingatia maslahi na maendeleo ya watumishi katika shughuli zake. Waajiri wamekuwa pia wakitambuliwa kwa kuwa na sera zinazozingatia ushindani wa kitaasisi, ubora wa kitija pamoja na kuwapo amani na utulivu sehemu za kazi.

Akizungumza katika hafla hiyo, Ofisa Mkuu wa Rasilimali Watu wa NMB, Emmanuel Akonaay, alisema tuzo za ATE walizoshinda ni miongoni mwa tuzo nyingi za ufanisi na ubora za kitaifa na kimataifa ambazo imezinyakua NMB mpaka sasa kwa mwaka huu wa 2023.

Kiongozi huyo aliongeza kuwa tuzo hizo pamoja na ufanisi wa utendaji kifedha uliopatikana mwaka huu hususani faida kubwa iliyopatikana umeufanya mwaka 2023 kuwa mwaka mwingine wa mafanikio makubwa kwa benki hiyo kubwa kuliko taasisi zote za fedha nchini.

Alikumbusha kuwa hivi karibuni, benki hiyo pia ilitunukiwa tuzo ya Mlipakodi Mkubwa nchini na ile ya taasisi inayoongoza kwa kuzingatia misingi na kanuni bora za ulipaji kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

"Hii inathibitisha namna ambavyo Benki ya NMB inashirikiana vyema na serikali pamoja na mashirika yake," Akonaay aliwaambia waliohudhuria hafla hiyo akiwamo Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndarichako, aliyemwakilisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Aliongeza kuwa NMB si tu ina wafanyakazi wengi bali pia inazingatia usawa wa kijinsia kazini ambapo kwa sasa wanawake ni asilimia 48 ya wafanyakazi wake wote.

**Tuzo nyingine ilizoshinda benki hiyo ni za mshindi wa pili wa Sekta Binafsi, wa kwanza katika Ubora, Tija na Ubunifu, na wa kwanza pia kwenye Masuala ya Usawa wa Kijinsia.**



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako (wa pili kushoto), akikabidhi cheti cha shukrani kwa Meneja Mwandamizi wa Rasilimali Watu wa GGML, Charles Masubi baada ya kampuni hiyo kuwa mmoja wa wadhamini wakuu wa hafla ya kukabidhi tuzo kwa mwajiri bora wa mwaka 2023, zilizoandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa GGML, Stephen Mhando, Mkurugenzi Mtendaji wa ATE, Suzanne Ndomba-Doran (wa pili kulia) na Mwenyekiti wa Bodi ya ATE, Oscar Mgaya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watendaji Jiji la Dar wajivunia utekelezaji miradi ya maendeleo

**Na Mary Geofrey**

WATENDAJI wa Jiji la Dar es Salaam wamebainisha mikakati yao ya kuinua uchumi na ustawi wa wananchi, wakijivunia utekelezaji wa miradi ya maendeleo unaofanywa na serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Katika ziara maalum ya kukagua miradi hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Jomaari Satula (pichani), alibainisha kuwa halmashauri inatekeleza miradi ya maendeleo.

Aliitaja miradi hiyo inajumuisha ujenzi wa barabara kwa ajili ya mabasi yaendayo haraka, maarufu mwendokasi, ujenzi wa madarasa kwa mfumo wa maghorofa katika Shule ya Sekondari Liwiti, ujenzi wa Shule ya Viziwi ya Uhuru Mchanganyiko, kituo cha afya cha kisasa cha Zingiziwa na kuendelea kufikisha huduma karibu na wananchi.

Mkurugenzi aliishukuru serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za ujenzi wa Soko la Kariakoo ambalo litaendelea kuwa kichocheo kikubwa cha ukuaji wa shughuli za kibiashara si tu katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, bali pia mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa kuwa ndio kitovu cha kupokea na kuuza bidhaa mbalimbali.

Alisema serikali chini ya uongozi wa Rais Samia, amepeleka fedha za kutekeleza miradi hiyo ya maendeleo kwenye sekta mbalimbali katika jiji hilo.

Ni hatua aliyoitaja inaakisi dhamira ya Rais kuboresha maendeleo na maisha ya wananchi ili kuwawezesha kujikwamua kiuchumi, pia kutatua kero katika sekta mbalimbali ikiwamo afya, elimu, mazingira, miundombinu na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

"Jitihada za serikali zimewezesha upatikanaji huduma mbalimbali kwa jamii kama vile hospitali, shule, masoko na barabara ili kukuza ustawi wa jamii na uchumi kwa wakazi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam," alisema.



Katika kuunga mkono jitihada hizo za Serikali Kuu, Mkurugenzi Satula alisema Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwenye bajeti yake ya mwaka 2023/24 na 2024/25, imetenga Sh. bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa masoko makubwa ya Ilala, Gongo la Mboto, Chanika na Mchikichini.

Pia imetenga Sh. bilioni 25 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya afya kama ujenzi wa vituo vya afya katika kata za Pugu Stesheni, Kisukuru na Buguruni, lengo likiwa ni kufikisha huduma muhimu karibu na wananchi na kuboresha huduma hizo katika jamii.

Alitaja vyanzo vikuu vya fedha hizo ni kutoka Serikali Kuu kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI, na fedha za ndani ya halmashauri hiyo inayolenga kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 120 katika mwaka huu wa fedha.

Mkurugenzi Satula aliwaahidi wakazi wa jiji hilo kuwa halmashauri itahakikisha inatumia vyema fedha kutoka Serikali Kuu na zinazokusanywa kutoka katika mapato ya ndani kama zilivyokusudiwa ili kuboresha ustawi wa jamii na ukuaji wa uchumi kwa wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, akizungumzia mikakati ya ulinzi na usalama, alisema wanahakikisha wananchi wanakuwa salama na kushiriki shughuli mbalimbali za uzalishaji mali, biashara na uwekezaji kama inavyohimizwa na serikali.

Kutokana na wilaya hiyo kupokea wageni wengi na biashara nyingi, Mpogolo alisema hawana budi kuhakikisha ulinzi na usalama wa wageni, wakazi wa Ilala na biashara zote zilizomo katika wilaya hiyo.

"Kwa muktadha huo, tumeendelea kushirikisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama katika kuhakikisha Wilaya ya Ilala inakuwa salama na kuvutia biashara na uwekezaji," alisema Mpogolo, ameongeza kuwa katika kuimarisha utawala bora, wameelekeza kila ofisi ya serikali ifikike na iwe na uwazi kwenye kutoa huduma kwa wananchi.

Vilevile, alisema wameshaelekeza taasisi zote za serikali wilayani Ilala ziwe na masanduku ya maoni ili kutoa fursa kwa wananchi kutoa maoni kuhusu utendaji kazi wa taasisi za serikali.

Katika kuhakikisha wilaya hiyo inaongeza ukusanyaji mapato, Mpogolo alisema wameweka mikakati mbalimbali ili wakusanye Sh. bilioni 120 mwaka huu wa fedha, wakidhibiti mianya ya ukwepaji kodi kwa kufanya sensa ya wafanyabiashara katika wilaya hiyo.


Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto alisema wamejipanga kuwapokea wanafunzi wanaoanza kidato cha kwanza, zaidi ya madarasa mpya 250 yamejengwa kuhakikisha kuwa wanapokea wanafunzi wote wanaotarajiwa kuanza masomo mwezi ujao kwa ngazi ya elimu ya sekondari.

Ofisa Elimu ya Awali na Msingi, Mwalimu Hussein Mgewa na Ofisa Elimu Sekondari, Mwalimu Mussa Ally, wakizungumza kwa nyakati tofauti, walieleza namna walivyojipanga kusimamia vizuri miradi ya elimu ili fedha za serikali zinazotolewa kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Dk. Zaitun Hamza alisema kuwa katika awamu hii ya serikali, halmashauri imefanikiwa kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati 15 inayojumuisha hospitali, vituo vya afya na zahanati.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MBAGALA | MAMU PHARMACY | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.151,KITALU 'Q10' HATI NAMBA 143195-KIBAMBA | AHMAD KASSIM OMARY | KIBAMBA | 13/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | NEZAK INVESTMENT LTD | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1019002 KIWANJA NAMBA P23439 KIFURU-KINYEREZI 2. NYUMBA YENYE HATI NA. 70437 KIWANJA NA. '213', KITALU '14' BUNJU KINONDONI | 1. ZACHARIA ANTHONY KAPAMA 2. DAFROSA ATHONY KAPAMA | 1.KIFURU KINYEREZI-ILALA 2.BUNJU KINONDONI | 13/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | WAWA COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 115345, KIWANJA NAMBA 124, KITALU '24' KIBADA KIGAMBONI 2.NYUMBA YENYE HATI NA DSMT1002975 KIWANJA NA. 2483, KITALU 'A' MBEZI MANYEMA, 3.NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.KND/KGG/KATI/214, KIGOGO KATI 4. NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOPO | 1.SALUM JUMA NYANDOTO 2. SALUMU JUMA NYANDOTO 3.SALUM JUMA MARWA 4.SALUMU JUMA NYANDOTO | 1.KIBADA- KIGAMBONI 2.MBEZI MANYEMA 3.KIGOGO KATI 4.KINZUDI GOBA | 15/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MAIN | TOMONI FARMS LIMITED | SHAMBA LENYE HATI YA MAUZIANO YA SERIKALI YA KIJIJI, EKARI 194 | FRANKLIN G. BAGALLA | KIJIJI CHA TOMONI-KIBITI RUFIJI | 14/12/2023 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KARIAKOO | LAMECK JOHN RUGIGA | 1.NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO 2.NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.59847 KIWANJA NA.2009 KITALU "D" | 1.LAMECK JOHN RUGIGA 2.CRISPIN PATRICK KAPILIMBA | 1.MBEZI MSHIKAMANO 2.SINZA | 14/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KINONDONI | VAM COMPANY LIMITED | NYUMBA | VENANT ANGELO BAKEMYA | BUNJU | 08/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | HASSAN RAMADHANI SHEKIKA | NYUMBA (2) | 1.HASSAN RAMADHANI HARASHI 2.HASSAN RAMADHANI SHEKIKA | 1.YOMBO DOVYA-MAKANGARAWE 2.TAMBANI MKURANGA | 07/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | HP PLANNERS & EVENTS MANAGEMENT LTD | NYUMBA (2) | 1.JAMES NDASKOI NNKO 2.DAPHROSER ABEID HAMZA | 1.TEGETA 2.KIGAMBONI | 20/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | YVONNE MAJEVU KUMBI | NYUMBA | AYUBU AUGUSTINO MSULE | KIBAMBA | 14/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | CESILIA SAMWEL KWEKA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | LEONARD JACOB NUBWA | MBAGALA KUU | 13/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | TUNU AMRUDINI MSHANA | NYUMBA | TUNU AMRUDINI MSHANA | VIWEGE KWA MPEMBA | 19/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | MOHAMED ABDALLAH LUTAMBI | KIWANJA CHENYE HATI MILIKI | MOHAMED ABDALLAH LUTAMBI | KIBAHA | 12/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | ABDULHMAN RAJABU MAHABA | NYUMBA | ABDULHMAN RAJABU MAHABA | ZINGIZIWA | 12/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | GEORGE JAPHET NDENGA | NYUMBA | GEORGE JAPHET NDENGA | KINYEREZI | 13/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | ONESMO PETER MASIMA | NYUMBA | ONESMO PETER MASIMA | UKONGA MAZIZINI | 13/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | MDAKI NASSORO KABELELE | NYUMBA | MDAKI NASSORO KABELELE | VIWEGE-MAJOHE | 12/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | VICTOR STEVEN MANG'ANA | NYUMBA | VICTOR STEVEN MANG'ANA | UKONGA | 14/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | ROBERT CHACHA NYAMBARI | NYUMBA | ROBERT CHACHA NYAMBARI | KITUNDA MTAA WA KINYANTIRA | 20/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | PAULO GIRIMBE RAWE | NYUMBA | PAULO GIRIMBE RAWE | KIVULE-ILALA | 14/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | KOKUBELWA PAUL NGAMBEKI | KIWANJA | ANTHONY AARON ICHWEKELEZA | MPIJI MAGOE | 15/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | BAHATI YOHANA NYATO | LYAMKENA-MAKAMBAKO | 15/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | NYUMBA ZENYE HATI YA MAUZIANO | FRENK SAMSON LEMAU | SHEWA-MBEYA | 13/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) ZENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | 1.MBEYA MJINI 2. TUNDUMA | 13/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | MWANJELWA , MBEYA MJINI | 13/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | EMANUEL MOYO MASETA | 1.NYUMBA (3) 2.KIWANJA | EMANUEL MOYO MASETA | 1.IFWEKENYE -MBOZI 2.SONGWE | 08/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | NDIMBWELU BANDEKISYE KAFWENDA | NYUMBA | PAULO KALOTA NDAWILA | NZOVWE-MBEYA | 12/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | IPYANA TIGER JUNIOR | NYUMBA | IPYANA TIGER JUNIOR | ILEMI-MBEYA | 12/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BRAITON REBEN MWANKEMWA | NYUMBA | BRAITON REBEN MWANKEMWA | IVUMWE | 18/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | IDD SALUMU HUSSEIN | NYUMBA | EDITH JOSEPH CHIWAMILA | ISYESYE | 18/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | CHARLES JOHN ZIMBA | NYUMBA | CHARLES JOHN ZIMBA | ITEZI -MASHARIKI | 20/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | KITETE-MBEYA | 11/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | MARIAM BATON MWANDENENE | NYUMBA | VUMILIA ELIAS NYAGAWA | NGOSI- MWAKIBITI | 19/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | FELIX SIMON MAVUMBO | NYUMBA | ZAWADI FABIAN KAHOHO | VIANZI- MKURANGA | 20/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MWANAHAMISI MSOFE BEDA | NYUMBA | MWANAHAMISI MSOFE BEDA | KIYOMBO- KITUNDA | 21/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MELANIA RAYMOND KILEWO | NYUMBA | MELANIA RAYMOND KILEWO | MIPEKO-TAMBANI MKURANGA | 20/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | ABDALLAH AHMAD MUHIDINI | NYUMBA | ABDALLAH AHMAD MUHIDINI | TEGETA 'A' - GOBA | 22/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | ALLY OMAR ALLY | NYUMBA | BAKARI FAKIH BAKARI | PUGU-KINYAMWEZI | 21/12/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | GRACE ADONIAS MTEGO | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.22 KITALU 'N' HATI NA.4870 | BLASIUS SWAI KAGINA | BUNDA | 21/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | ABAS HAMAD ISSA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PETER NDULU MAHARAGE | MISUNGWI-MWANZA | 20/12/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARIA JOHN PETRO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JOHN PETRO KALISA | KILOLELI 'B' - MWANZA | 20/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.NYUMBA 2. KIWANJA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.IGELEGELE BUGARIKA 2. BUJINGWA-MWANZA | 15/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | SELEMANI CHARLES MNIKO | NYUMBA | SELEMANI CHARLES MNIKO | MBUGANI -MWANZA | 19/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | EMMANUEL LUKINDA LUTIMA | BUS TATA T847 DKN | EMMANUEL LUKINDA LUTIMA | MWANZA MJINI | 19/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JOSEPH MAKALA MAKALA | NYUMBA | JOSEPH MAKALA MAKALA | NYASAKA ILEMELA MWANZA | 20/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JAMES JACOB KALULEMA | NYUMBA | JAMES JACOB KALULEMA | MAHINA KANYERERE-MWANZA | 20/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | JOSTER JACKSON NSASHE | NYUMBA | KERAMBO CHOGO KERAMBO AND JOASTER | KITUNDA MZINGA | 14/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | MHINA JOSEPH KWELLA | NYUMBA | MHINA JOSEPH KWELLA | PUGU | 14/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | RAYSONS AND COMPANY | NYUMBA | RAYMOND MICHAEL MREMI | KIBAHA | 12/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | DAVID RIGHTON MINGA | NYUMBA | DAVID RIGHTON MINGA | KILUVYA | 12/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | AMINA CLEMENS NAZA | NYUMBA | ABASI ZUBERI CHANZI | KIBAMBA KIBWEGERE | 13/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | ALBERTO SHEDRACK KUMWILU | NYUMBA | ALBERTO SHEDRACK KUMWILU | MBEZI LUIS | 13/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | MLIMO COMPANY LTD | NYUMBA | TIMOTH ANISETH KATWELA | KIMARA TEMBONI | 14/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | MSIBA RAYMOND MSIBA | NYUMBA | MSIBA RAYMOND MSIBA | KILUVYA | 14/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | OBEDI ZIHIRWADI MSINGA | NYUMBA | OBEDI ZIHIRWADI MSINGA | KIBAHA KWA MATHIAS | 14/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | MTUMWA SALUM HAMAD | NYUMBA | MATONGO NKWABI NSWAGA | KIGOGO | 21/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | AMANI OMARI NOMBWANI | NYUMBA | AMANI OMARI NOMBWANI | KIGOGO-KIGAMBONI | 11/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TANDALE | MAIMUNA ISAYA KIRINDO | NYUMBA | MAIMUNA ISAYA KIRINDO | MJI MPYA | 28/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | PADONI KIBAYU SIMON | NYUMBA | PADONI KIBAYU SIMON | MAJOHE | 20/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | ALLY SHAWEJI OMARY | NYUMBA | ALLY SHAWEJI OMARY | KIBAMBA | 12/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TANDALE | SALUM RAJABU MCHOMVU | NYUMBA | SALUM RAJABU MCHOMVU | KICHANGANI- MAJOHE | 21/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | EDNA ISHENGOMA RWEMILINZI | NYUMBA | EDNA ISHENGOMA RWEMILINZI | TEGETA 'A' | 20/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | YOVANALI SAIMONI MAGIGE | NYUMBA | YOVANALI SAIMONI MAGIGE | GONGO LA MBOTO | 27/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | OLIVA STANLEY MNDEME | NYUMBA | OLIVA STANLEY MNDEME | KIMANDOLU -ARUSHA | 20/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | Dominick Losinyari Noah | NYUMBA | Dominick Losinyari Noah | Kibamba | 20/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | Chitegetse Monica Migembe | NYUMBA | Chitegetse Monica Migembe | Bunju | 20/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | Mlopa Idrisa Sadallah | KIWANJA | Mlopa Idrisa Sadallah | Makurunge-Bagamojo | 20/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | Nelson Peter Shoo | KIWANJA | Nelson Peter Shoo | Bokotimiza-Kibaha | 21/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | Adam David Kessy | VIWANJA (2) | Adam David Kessy | 1.Kisopwa Kwembe 2. Kisarawe Pwani | 22/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | Celestine Msimbu Shija | KIWANJA | Celestine Msimbu Shija | Bokotimiza-Kibaha | 21/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | Jordan Joseph | KIWANJA | Jordan Joseph | Mbezi Muhongo | 22/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | Annaneema Daniel Ritte Ritte | KIWANJA | Annaneema Daniel Ritte Ritte | Segu Chini- Dodoma | 22/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | Samwel David Bagenda | KIWANJA | Samwel David Bagenda | Mbagala Kuu Kijichi | 27/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | Ibrahim Kenneth Nyamubi Nyamubi | KIWANJA | Ibrahim Kenneth Nyamubi Nyamubi | Kimara Mavurunza | 28/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | Hamis Abasi Sapi | KIWANJA | Hamis Abasi Sapi | Mwembe Bamia- Chamanzi | 29/12/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | Dennis Deusdedit Kashasha | KIWANJA | Dennis Deusdedit Kashasha | Bagamoyo | 20/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0715868000/ 0714939933/0785242219/ 0759282344/0787129539/ 0767808848/ 0714208208
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha **kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.**

177434

# ICTC yapeleka wabunifu 7 kongamano la Algeria

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha inakuza ubunifu kwa kampuni changa za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) nchini, Tume ya TEHAMA (ICTC) imefanikisha safari ya wabunifu saba kwenda Algiers, Algeria kushiriki katika kongamano la siku tatu la kimataifa la TEHAMA barani Afrika litakaloshirikisha zaidi ya mataifa 50 lililoanza jana.

Wabunifu hao wa Kitanzania watapata fursa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutangaza kazi zao, kukutana na wataalamu wengine wa TEHAMA kutoka sehemu mbalimbali duniani ambako wanatarajiwa kujifunza kuelekea katika ukuaji wao kisekta.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA, Dk. Nkundwe Mwasaga, akizungumza jana jijini Dar es Salaam, alisema kuwa Tume na taifa kwa ujumla, kongamano na maonesho hayo ni faida kubwa kwa nchi kwa kuwa vitasaidia kukuza na kuvutia uwekezaji nchini.

"Hiyo ni hatua kubwa kwetu kama Tume ya TEHAMA, lakini kwa nchi. Haya ni matunda ya uratibu wa programu ya kukuza kampuni changa za TEHAMA (ICT Startups) ili kuwezesha bidhaa za TEHAMA kuingia katika soko na kuchangia katika kukuza uchumi na kutengeneza ajira kwa vijana. Tume imewezesha kampuni changa kadhaa kuanza kutoa huduma," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Mwasaga, ushiriki katika kongamano hilo kubwa Afrika umewezeshwa na ICTC. Aliishukuru serikali kwa kuipa nguvu sekta ya TEHAMA katika mpango wa kujenga uchumi wa kidijitali, kwa kuwa umechangia kwa kiasi kikubwa kufanikisha safari ya wabunifu hao.

Kongamano hilo linalotarajiwa kuhudhuriwa na wabunifu 500, watazamaji zaidi ya 10,000, wawekezaji 200, wabobezi katika sekta ya Tehama wapatao 100, kampuni za Tanzania zinazotarajiwa kushiriki ni Ngasmake (Lipa kwa Ngasmake (Lipa kwa Uhakika), Niajiri, Neuro-Sarufi AI, Simplitech, Mipango App, Scancode na Settlo. Benki ya CRDB iliyoingia makubaliano na Tume ya Tehama kuendeleza Wabunifu wa Kampuni ndogondogo za TEHAMA kupitia programu ya Imbeju, pia ni sehemu ya washiriki.

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Ufundi wa Tume ya TEHAMA ambaye yuko Algeria na wabunifu hao, Jasson Ndanguzi, aliyemwakilisha Mkurugenzi Mkuu, akizungumzia manufaa ya ICTC kushiriki katika kongamano na maonesho hayo, alisema ni pamoja na kusaidia kuvutia na kuongeza fursa za uwekezaji mitaji katika kampuni bunifu za TEHAMA nchini.

"Pia kuna fursa ya kuongeza ujuzi wa programu za uanzishwaji wa vituo vya bunifu za TEHAMA nchini kwa kujifunza kutoka nchi zingine zinazoshiriki kongamano hilo, kupata washirika wa kuendesha programu za ubunifu wa kidijitali na kukuza soko la bidhaa za TEHAMA zinazotokana na bunifu za TEHAMA ili kukuza pato la taifa, lakini kutangaza nafasi ya Tanzania katika uwanda wa masuala ya bunifu za kidijitali.

Ukuzaji na kuvutia uwekezaji ni moja ya majukumu ya Tume inayotekeleza Sera ya Taifa ya TEHAMA pamoja na sera nyingine zinazohusiana na kuendeleza matumizi yake, lengo likiwa kutengeneza ajira na kuchangia shughuli za kiuchumi na kijamii, huku ikiimarisha uratibu wa shughuli za TEHAMA ili kuongeza mchango wa sekta husika katika uchumi wa taifa.

Tume, kwa sasa inaelekeza nguvu kuanzisha vituo vya ubunifu wa TEHAMA kote nchini, ikianza na mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Dodoma, Tanga, Mbeya, Lindi na Zanzibar, lengo likiwa kusogeza huduma karibu na wananchi, hasa ikizingatiwa kumekuwa na ongezeko la uhitaji wa matumizi ya Teknolojia kwenye uchumi wa Tanzania.

# Wahasibu wachangia milioni 15/- matibabu watoto wenye saratani

**Na Elizabeth Zaya**

WASHIRIKI wa kongamano la Wahasibu na Wakaguzi, wametoa Sh. milioni 15 kwa ajili ya kuwasaidia watoto wanaougua magonjwa ya saratani katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Akizungumza kwa niaba ya washiriki wa kongamano hilo baada ya kutoa msaada huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi hiyo ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA), Pius Maneno, alisema umechangwa na wanataaluma hao ikiwa ni sehemu ya mchango wa huduma yao kwa jamii.

"Tunatoa pongezi kwa maboresho makubwa yanayofanyika Muhimbili, kwa kweli nchi yetu inafanya kazi kubwa hususani katika kuboresha huduma kwa wananchi wake na sisi tunapopata nafasi tunapaswa kuunga mkono juhudi hizi," alisema Maneno.

Kaimu Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dk. Julieth Magandi, alisema fedha hiyo itasaidia kwa kiwango kikubwa kuchangia matibabu kwa watoto hao wanaougua saratani katika hospitali hiyo na kwamba kwa siku wagonjwa wanaohudumiwa ni 6,000, Mloganzila ni 1,500 na Muhimbili ni 4,500.

Alisema kwa mwaka, hospitali hiyo imekuwa ikitoa misamaha ya Sh. bilioni 1.7 asilimia tisa mpaka 10 ya misamaha hiyo ni kwa ajili ya watoto wanaougua saratani ikihusisha malazi, dawa, vipimo na Radiolojia.

"Kwa hiyo tunatoa wito kwa wadau wengine kuendelea kuwasaidia wagonjwa na tunaamini kwamba bima ya afya kwa wote itakuwa ni suluhisho kwa magonjwa kama haya na tunaishukuru serikali kwa hilo."

Mmoja wa washiriki wa kongamano hilo, Aisha Salum, alisema wameguswa kuwachangia watoto hao sehemu ndogo ya gharama za matibabu yao.



# TCFPA yakabidhi vitanda 24 Hospitali ya Wilaya Muheza

Na Steven William, MUHEZA

TAASISI ya Tanzania China Friendship Promotion Association (TCFPA) imekabidhi msaada wa vitanda 24 vyenye thamani ya Sh. 16,176,948 katika Hospitali ya Wilaya ya Muheza mkoani Tanga.

Vitanda hivyo vilikabidhiwa juzi na Mwakilishi wa Taasisi hiyo, Husna Sharif katika hafla iliofanyika katika hospitali hiyo na mgeni rasmi alikuwa Mbunge wa Muheza, Hamisi Mwinjuma.

Akikabidhi vifaa hivyo Husna alisema msaada huo umetolewa ili kusaidia wagonjwa ambao wanahitaji huduma ya kulazwa.

Alisema, kuwa taasisi hiyo imekuwa ikisaidia kutoa misaada mbalimbali katika sekta ya elimu na afya ikishirikiana na Serikali ya China kupitia ubalozi wao hapa nchini ili kumuunga mkono Rais Samia Suluhu.

"Kwa kidogo ambacho tulichokipata tumeamua tukitumie kusaidia jamii katika Wilaya ya Muheza kwa kutoa msaada wa vitanda katika Hospitali ya Wilaya ya Muheza ya Samia Suluhu," alisema Husna.

Awali akitoa taarifa ya hospitali hiyo Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Tanga, Dk. Juma Mombokaleo alisema hospitali hiyo inahudumia wakazi wengi na imepata vifaa vya kisasa.

Naibu Waziri Hamisi Mwinjuma aliishukuru taasisi hiyo kwa kutoa msaada hiyo kwa kuwa itasaidia kuboresha huduma ya afya katika hospitali hiyo.

# Watakaopandisha bendera Mlima Kilimanjaro kupata intaneti bure

Na Godfrey Mushi, MOSHI

SHIRIKA la Mawasiliano Tanzania (TTCL), limejitosa kubeba gharama za huduma zote za mawasiliano ya intaneti bure kwa wazalendo 204 watakaopandisha Bendera ya Taifa katika kilele cha Uhuru cha Mlima Kilimanjaro, kuelekea maadhimisho ya miaka 62 ya uhuru wa Tanganyika.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa TTCL, John Yahaya, aliyasema hayo jana kabla ya wazalendo hao kuanza safari ya kupanda mlima huo, kupitia kampeni ya twenzetu kileleni 2023.

Alisema uwepo wa huduma hiyo itakuwa ni fursa ya kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo katika hifadhi ya mlima wetu, ndani na nje ya nchi yetu, lakini itahamasisha Watanzania kujenga mazoea ya kutembelea vivutio vya Mlima Kilimanjaro na maeneo mengine ya utalii.

Alisema tukio hilo linaunga mkono juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, kuimarisha umoja na mshikamano ndani ya nchi yetu, katika kukuza sekta ya utalii sambamba na kuimarisha mawasiliano nchini.

Alisema, shirika hilo limeendelea kutekeleza mkakati wake wa kuimarisha mawasiliano nchini kwa kuhakikisha kunakuwapo na miundombinu ya kisasa na yenye uwezo mkubwa katika kutoa huduma ndani na nje ya Tanzania.

Alisema katika safari hiyo itakayoanza kesho shirika hilo kwa kutambua umuhimu wake, itatoa huduma ya intaneti bure kwa washiriki watakaopanda mlima huo katika kipindi hiki cha kampeni ya twenzetu kileleni.

"Washiriki wote watakaopanda Mlima Kilimanjaro, katika kipindi hiki cha kampeni ya twenzetu kileleni, watapata fursa hiyo bure wafikapo kila kituo katika mlima huo, ili kutambua umuhimu wa maadhimisho haya ya miaka 62 ya uhuru wa nchi yetu.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Jenerali Mstaafu, George Waitara, aliwataka Watanzania kuendelea kuutangaza mlima huo kwa kutumia fursa mbalimbali zilizopo hasa katika kipindi hiki cha kuelekea kwenye maadhimisho ya miaka 62 ya uhuru wa Tanganyika.

"Utaratibu huu wa kupanda mlima wakati wa kusherehekea uhuru wa nchi yetu, ulianza mwaka 2008 na sasa ni miaka 15 imepita, nafurahi kila mwaka mwitikio unakuwa ni mkubwa, na mwaka huu nimeambiwa tuko 200, hii ni hatua kubwa sana na watu wameitikia."

Aliwasisitiza wanaopanda mlima huo kuuheshimu kwa kufuata maelekezo na taratibu zote wanazopewa kwa wale wasimamizi wao ili kuepuka kupata madhara.

Akimwakilisha Mkurugenzi wa Makampuni ya utalii ya Zara Tours, Ibrahim Othman Jama, alisema idadi ya watakaopanda mlima mwaka huu ni 200 kutoka katika mashirika na taasisi mbalimbali.

Alilishukuru TTCL kwa kutoa huduma za mawasiliano katika mlima Kilimanjaro, kwa kuwa itaharakisha huduma za mawasiliano kwa wale watakaokuwa mlimani.

"Tunamshukuru Rais wetu, Samia Suluhu Hassan kwa kupitia filamu yake ya 'The Royal Tour' ambayo imeweza kuleta matunda mengi kwa kutangaza vivutio vyetu vilivyopo hapa nchini."



Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo na Mbunge wa Jimbo la Muheza, Hamisi Mwinjuma (kushoto), akizungumza na wanafunzi kutoka shule nne za sekondari; Misozwe, Bwembwera, Songa na Kwabutu, baada ya kuwakabidhi msaada wa baiskeli 203, wilayani Muheza mkoani Tanga juzi, ili kuwarahisishia usafiri wa kwenda shuleni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Rais Samia atoa magari Mount Meru

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

RAIS Samia Hassan Suluhu ametoa magari manne ya kubeba wagonjwa na huduma za afya, pia lori kwa ajili ya kliniki tembezi yenye thamani ya Sh. milioni 646 katika Hospitali ya Mount Meru iliyoko Halmashauri za Wilaya ya Longido, mkoani Ngorongoro.

Akikabidhi magari hayo jana jijini Arusha, Mkuu wa Mkoa huo, John Mongella alisema kliniki hiyo tembezi ianzie wilayani Ngorongoro, ili wananchi wapate huduma za afya katika kata na vijiji mbalimbali wilayani hapo na wilaya nyinginezo kadri ratiba itakavyopangwa.

Alisema Rais Samia anajitahidi kuboresha sekta ya afya ikiwamo kutoa magari hayo, kwa ajili ya kusaidia wananchi kupata huduma za afya pale walipo hivyo yatumike kwa malengo kusudiwa na si kubebea watu wasiohusika.

"Serikali inatekeleza ahadi zake kwa vitendo, magari haya ya wagonjwa yapo matatu na jiografia ya Mkoa wa Arusha kuna maeneo yana changamoto za ufikaji wake na utoaji huduma za afya ni changamoto, hivyo nawashukuru wabunge wa mkoa huu, kwa kupitisha bajeti kadhaa zilizozaa matunda haya," alisema.

Aliagiza magari hayo yatunzwe na yawe chini ya usimamizi wa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Dk. Charles Mkombachepa, atakayepanga ratiba nzima ya mzunguuko wa kliniki inayotembea, kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi.

Naye Mganga Mkuu wa Hospitali ya Mount Meru, Mkombachepa aliishukuru serikali kwa kuboresha huduma za afya ikiwamo utoaji wa magari hayo, ambayo yataendelea kuokoa maisha ya wananchi, ikiwamo wagonjwa wa dharura, kinamama wanaojifungua ikiwamo watoto wachanga wenye changamoto.

Awali Mbunge wa Ngorongoro, Emmanuel Shangai, alisema magari hayo yataondoa changamoto za wananchi wa Ngorongoro, ambao wanakaa mbali na vituo vya afya na kuna wakati magonjwa ya mlipuko ikiwamo surua huwasumbua watoto katika maeneo yaliyopo pembezoni.

"Tulikuwa tukipatiwa huduma za afya kwa kutumia ndege katika maeneo yasiyofikika, lakini sasa hivi ndege hiyo imekuwa changamoto sababu ya vibali, hivyo upatikanaji wa gari la wagonjwa na hii kliniki inayotembea itawezesha wananchi kupata huduma za afya kadri ratiba ilivyopangwa," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Marko Ng'umbi, alisema wilaya hiyo ina zaidi ya vituo vitano vya afya, lakini jiografia yake na mtawanyiko maeneo ya pembezoni, ni changamoto na ilikuwa haina gari la wagonjwa.





# Nyumba Ntobhu chanzo maambukizi UKIMWI

**Na Timothy Itembe,** MARA

UTAMADUNI unaoendelea katika kabila la Wakurya, mkoani Mara ya mwanamke kuoa mwanamke mwenzake maarufu kama 'Nyumba Ntobhu' imetajwa kuwa chanzo cha maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI mkoani Mara.

Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Michel Mtenjele, kufuatia elimu ya kudhibiti na kukabiliana na ugonjwa huo inayoendelea kutolewa wilayani humo na kuisihi jamii kubadilika kwa kuwa desturi hizo zimepitwa na wakati.

Mtenjele alisema Nyumba Ntobhu yenye maana ya nyumba bila mwanamume ambayo inamlazimu binti aliyeolewa na bibi kufanya ngono zembe na wanaume tofauti lengo likiwa ni kulinda ndoa ya bibi husika kwa kumzalia watoto zimepitwa na wakati.

Mkuu huyo wa wilaya pia alikemea vitendo vya ukeketaji kwa watoto ambavyo vinatajwa kuendelea kufanyika kwa siri licha ya kupigwa vita kitaifa na kimataifa na kuwataka kuacha usiri katika mambo yenye viashiria vya kuongeza maambukizi ya ugonjwa huo ili kurahisisha vita hiyo.

Mratibu wa Ukimwi Halmashauri ya Wilaya ya Tarime Vijijini, Dk. Joel Mabara, alisema kiwango cha maambukizi ya virusi hivyo ni miongoni mwa waliopimwa kimepungua kutoka asilimia mbili mwaka 2022/2023 hadi kufikia 1.7 Oktoba 2023.

Alitaja idadi ya watumiaji wa dawa za kufubaza virusi kuwa mpaka Oktoba 2023 walifikia 4,549 na jitihada mbalimbali zinaendelea kufanyika ili kupunguza maambukizi ya VVU ikiwamo kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa kujifungua.

Meneja Uhusiano wa Mgodi wa Barrick North Mara uliopo Nyamongo, Francis Uhadi, alisema wanatambua umuhimu wa Afya Bora kwa jamii hali inayowasukuma kushiriki katika mapambano dhidi ya Ukimwi huku wakianzia upimaji kwanza kwa wafanyakazi wao.

Uhadi alisema mpaka sasa kuna miradi ya Sh.bilioni 7.3 inaendelea kutekeleza kwa jamii na kuwa wanamkakati wa kuvifikia vijiji vyote vinavyozunguka mgodi kama sehemu ya kurudisha kwa jamii.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, akimkabidhi tuzo ya ushindi wa jumla Ofisa Raslimali Watu Mwandamizi wa Barrick North Mara, Eric Wambura (katikati) na Meneja Raslimali Watu wa Mgodi wa Bulyanhulu, Lumbu Kambula (kushoto), wakati wa hafla ya Chama cha Waajiri Tanzania, Dar es Salaam jana. Kampuni ya Barrick mbali na ushindi wa jumla imenyakuwa tuzo nyingine tano. Wengine ni wafanyakazi wa kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi Shinyanga waonywa uharibifu miundombinu ya maji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI mkoani Shinyanga ambao wametekelezewa miradi ya majisafi na salama katika maeneo yao, wametakiwa kuitunza miundombinu ya miradi hiyo ili itoe huduma kwa muda mrefu na kuondoa kabisa adha ya kutumia maji yasiyo safi na salama.

Ombi hilo limetolewa juzi na Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Mkoa wa Shinyanga Grace Bizuru, katika mwendelezo wa ziara ya umoja huo kukagua utekelezaji wa miradi ya maji kwa wananchi, wakiwa wameambatana na Mbunge wa Viti Maalum mkoani humo, Santiel Kirumba.

Akizungumza baada ya kukagua miradi hiyo katika halmashauri wilayani Kahama na Shinyanga, Grace aliwataka wananchi kutoharibu kwa namna yoyote miundombinu hiyo na kuilinda ipasavyo kuifanya adhima ya serikali ya kumtua mama ndoo kichwani kuwa endelevu.

"Tunzeni miundombinu hii kwani serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika utekelezaji wa miradi hii hakikisheni lengo la serikali linatimia wakati wote bila kuifanyia hujuma ya aina yoyote," alisema Grace.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) wilayani Kahama, Mhandisi Paschal Mnyeti, awali akisoma taarifa ya utekelezaji wa mradi huo wa Nduku hadi Busangi alisema utanufaisha wananchi 11,300 na sasa upo asilimia 60 na gharama zake ni Sh. bilioni 5.3.

Naye Meneja RUWASA wilayani Shinyanga, Mhandisi Emmael Nkopi, awali akisoma taarifa ya mradi wa Maji Masengwa, alisema utanufaisha wananchi 24,252 na utagharimu Sh. bilioni 4.7. Tayari umekamilika na kwamba katika mradi wa maji Kijiji cha Kilimawe unahudumia wananchi 2,262 na gharama zake ni Sh.milioni 333.1.

Mbunge wa Viti Maalum mkoani Shinyanga, Santiel Kirumba, ametumia fursa hiyo kumpongeza Meneja wa RUWASA mkoani humo, Mhandisi Julieth Payovela, kwa kusimamia vyema utekelezaji wa miradi ya maji, ambayo mingi imeshakamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

## Smart Mwenyekiti mpya CCM Mwanza

**Na Waandishi Wetu,** MWANZA

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Misungwi, Masanja Lushinge maarufu Smart, ameibuka kidedea katika uchaguzi wa Mwenyekiti wa chama hicho ngazi ya Mkoa na kuchukua nafasi ya Reuben Sixbert aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Masasi.

Akitangaza matokeo hayo katika Ukumbi wa CCM Kirumba jijini Mwanza, Mjumbe wa NEC, Saidi Mtanda ambaye alikuwa msimamizi wa uchaguzi huo alisema Lushinge aliibuka mshindi kwa kura 784 kati ya 1151.

Mtanda alisema kura 28 ziliharibika na kufanya kura halali kuwa 1,183 zilizopigwa na wajumbe wa uchaguzi huo kati ya wagombea watano ambao ni Sabana Lushu aliyepata kura 257, Mayala Mulongo kura 20, Elizabeth Watson kura 7 na Dk. Angelina Samikea aliyeambulia kura 15.

Akizungumza baada ya kutangazwa mshindi Lushinge aliahidi kushirikiana na wana CCM wote mkoani hapa kufanikisha uchaguzi wa mwaka 2024 wa wenyeviti, wabunge, madiwani na Rais wa mwaka 2025.

"Naomba niwashukuru wajumbe wote mlionipa kura lakini wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa kwa kupitisha jina langu," alisema Smart.

Alisma CCM Mkoa wa Mwanza inajumla ya wajumbe 1,183 ila baada ya kuteuliwa kwa Sixberb Jichabu wamebaki wajumbe 1,182 lakini waliohudhuria mkutano huo ni wajumbe 1,155 na waliopiga kura ni 1,111 na kuwezesha kumpata mwenyekiti atakaye ongoza kwa miaka mitano hadi 2027.

Aliyekuwa Mwenyekiti wa muda na Mjumbe wa NEC Mkoa wa Mwanza, Jamal Abdul, alisema, wajumbe wao wamemchagua kiongozi wanayeamini kuwa atatenda haki kwa wanachama wote.

"Uchaguzi umekwisha, wajumbe mmemchagua mnayemtaka, hatutaki kuwe na nyufa za makundi na mpasuko, tukilee chama, Mwanza ni dira ya siasa Kanda ya Ziwa, inatazamwa kwa jicho la tatu," alisema Jamal.

Reuben Sixbert alichaguliwa mwaka 2022 na kudumu madarakani kwa muda wa mwaka mmoja na baadaye kuteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuwa Mkurugenzi wa Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara kuchukua nafasi ya aliyekuwa Mkurugenzi wa Wilaya hiyo Erica Yegella aliyepangiwa majukumu mengine.

**Imeandaliwa na Thomas Wandiba, SAUT na Rose Jacob, MWANZA**



Ukurasa 12

**Samatta sauti itangazayo umuhimu wa utawala bora, haki na sheria**



Ukurasa 13

Mabadiliko tabianchi Dubai yanapoanza na mguu mzuri



Ukurasa 14

**UJIO SOMALIA EAC**

**Haya ni muhimu; mosi mwanachama kulipa ada, jumuiya kujitegemea**

siasa

JUMATANO DESEMBA 6, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

WOSIA WA JENISTA WANAHABARI

# Wanawake wasijidogoshe wanaweza adui yao ni mwanaume mpinga maendeleo

- Awakumbusha hata Rais Samia ni TAMWA

**Na Gaudensia Mngumi**

WANAWAKE wa Tanzania wamethibitisha kuwa wanapopewa kijiti wanakimbia mwanzo hadi mwisho na kuibuka washindi kwenye riadha bila kukwama wala kutazama nyuma.

Ni jambo la kushangiliwa na kusherehekewa, ndicho kinachofanyika hivi karibuni wakati wa kuadhimisha miaka 36 ya Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA),kilichoanzishwa 1987 kutetea haki za wanawake, wasichana na watoto kupitia vyombo vya habari, lakini pia kupaza sauti ili kuwa na taifa linaloongozwa kwa mrengo wa usawa wa jinsia.

TAMWA tangu kiliposhika kijiti kimefanikiwa mambo mengi kuanzia kupaza sauti za wanawake, kuwahamasisha kuwa viongozi, kuibua matatizo yao mijini na vijijini na kufanikisha kubadilishwa na kutungwa sheria zenye mrengo wa kuleta usawa na ulinzi kwa wote.

TAMWA ilipozaliwa ililenga kupunguza umaskini na migogoro mbalimbali iliyoathiri zaidi wanawake na watoto na taifa kuanzia unyanyasaji, elimu duni, mila kandamizi kama ukeketaji, kurithi wajane na ndoa utotoni yote hayo yakiwaumiza wanawake.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhagama, akiwa na wanachama, kutafakari safari ya mafanikio kwa miaka 36, anasema wanawake wasijidogoshe wanashinda mbio kuanzia mwanzo hadi mwisho naye ni shuhuda.

"Wanawake tunaweza kufanya mambo makubwa siyo mpaka tuwezeshwe hapana, tunaweza tupewe nafasi. Sisi ni watu muhimu kwenye jamii. Tena niwaambie Rais Samia Suluhu Hassan anawatazama wanawake wanahabari kama jicho muhimu kwa maendeleo ya taifa," anaongeza



Mkurugenzi wa Mfuko wa Wanawake Rose Marando (kushoto), viongozi wa TAMWA, Mkurugenzi Dk. Rose Reuben, Mwenyekiti, Joyce Shebe (kulia) akimpongeza Waziri Jenista Mhagama wakati wa sherehe ya mafanikio. **PICHA: TAMWA**

Waziri Jenista, akimwakilisha Rais, aliyekusudiwa kuwa mgeni rasmi.

"Ni jambo la kufurahisha Mama wa Taifa Samia ni mwana TAMWA, amefanyakazi na shirika hili wakati akiwa Waziri wa Kazi, Jinsia na Watoto Zanzibar..."

Anasema pamoja na Rais Samia yeye pia ni zao la TAMWA, shirika likishiriki kumuibua, kumfunda , kumnoa na kumjengea uwezo hadi kuingia kwenye siasa ili kuongeza ushiriki mkubwa wa wanawake kwenye vyombo vya maamuzi.

"TAMWA imelea wanawake wanasiasa, tena inashirikiana na wanawake wabunge. Ni sehemu ya maisha yangu na Rais wetu pia..."anasema, akisisitiza wanawake hawajawahi kushindwa harakati za kupata usawa wa kijinsia.

Anawakumbusha wana TAMWA kuwa ni lazima kuendelea kupambana ili idadi ya wanawake iwe kubwa kwenye 'board room' vinginevyo itakuwa vigumu kufikia 50/50 au usawa wa kijinsia wanaoutamani.

"Lazima tufanye bidii zaidi kumlinda mwanamke kiongozi, ili kuleta mabadiliko miaka 62 ya uhuru hatujapata kiongozi mwanamke lakini leo tunaye Rais Samia, lazima tuulinde uongozi wa mwanamke" anasisitiza.

Akizungumza kwa niaba ya Rais anasema ulinzi wa mwanamke kiongozi utafanikishwa kwa kuamua kuwa bila kujali itikadi za vyama wala mrengo wa kisiasa, kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka ujao na ule mkuu wa 2025 kutekeleza mkakati wa kijinsia wa kuunga mkono na kuwapa kura wagombea wanawake.

"Kama tutaamua mkakati wa usawa wa kijinsia utafanikiwa kwa kuwapata wanawake viongozi na wawakilishi wengi kwenye vyombo vya maamuzi,"anasema Waziri.

Anakumbusha kuwa kati ya ajenda muhimu kwa wanawake zinazoshughulikiwa ni pamoja na afya bora ya uzazi, matibabu ya wanawake na watoto ambayo Rais Samia anayasimamia kwa kuongeza hospitali zikiwamo huduma za kibingwa ili kufikia afya bora ya kinamama.

Aidha, anasema suala jingine ni elimu kwa wanawake ambayo pia anaisimamia ikiwarudisha shuleni wasichana waliokwama wakiwamo waliopata mimba ututoni , kuongeza madarasa na kusogeza elimu karibu na wananchi, bila kusahau kuongeza huduma ya maji maji mijini na vijijini.

**VIONGOZI BORA**

Anasema wanawake viongozi wanahitajika maana ni watendaji bora, si wala rushwa tena hawataki kuharibu kazi. Wanajenga ndoto na kuzisimamia hadi kuzitekeleza na zaidi wanaweza kufanyakazi nyingi kwa wakati mmoja bila kulalamika na kuchoka.

**INAENDELEA UK. 12**

# Samatta sauti itangazayo umuhimu wa utawala bora, haki na sheria

• Ni somo kupitia kitabu alichoandika




Uzinduzi wa kitabu cha Utawala Bora cha Jaji Mkuu mstaafu Barnabas Samatta (wa pili kulia), aliyeongoza kuanzia 2000 hadi 2007. **PICHA: SABATO KASIKA**

**Na Sabato Kasika**

JAJI Mkuu mstaafu Barnabas Samatta, amezindua kitabu alichoandika akikiita 'Utawala Bora. Vita dhidi ya udhalimu, rushwa na elimu duni' na ujumbe wake kwa taifa ni kuwapo haki na amani ndani ya nchi, ambavyo huletwa na haki iliyomo kwenye sheria.

Kikihaririwa na Mkurugenzi mstaafu wa Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Afrika (WILDAF), Dk Judith Odunga, anakifanyia uchambuzi na kueleza baadhi ya mambo muhimu, wakati wa uzinduzi uliofanyika Dar es Salaam wiki iliyopita, ukishuhudiwa pia na Jaji Mkuu, Profesa Ibrahim Juma, wataalam wa sheria na wadau wa haki za binadamu.

Katika uzinduzi huo, Dk, Judith anasema, maudhui ya kitabu hicho yamepangwa katika sura kumi, zinazoelezea kwa undani mada mbalimbali ya kwanza ikigusia utawala bora unaohusu sheria.

"Lakini kitabu hiki pia kinaelezea faida kuu za utawala bora, utawala bora na utawala wa sheria, aina za viongozi na maendeleo ya watu, usawa wa kijinsia, serikali bora na sekta zake kuu, uovu wa rushwa, matunda ya msingi wa utawala bora na utawala wa sheria na maana ya katiba ya nzuri ndani ya nchi," anasema Dk. Judith.

> Lakini pia haki ya wananchi kuheshimiwa na uongozi wa nchi yao, haki yao ya kushirikishwa katika maamuzi mbalimbali yanayohusu nchi yao.

Mhariri anasema Jaji Samatta anaelezea maana ya utawala bora kuwa ni utawala wa kisheria unaoheshimu haki za binadamu, uwajibikaji wa serikali katika maamuzi na utekezaji wa majukumu yake.

"Uadilifu miongoni mwa viongozi kwa mujibu wa katiba ya nchi na uwazi, lakini pia anazungumzia kuhusu uwapo wa uaminifu, kwa kuzingatia misingi ya utawala wa sheria ambayo watu wote bila kujali nafasi zao wanatakiwa kuizingatia," anasema.

Dokta Judith anasema, katika kitabu hicho, Jaji Samatta anafafanua kuwa utawala bora unajumuisha mambo mbalimbali ikiwamo uhalali wa uongozi wa nchi, kuanzia serikali iliyochaguliwa na wananchi kihalali, ushirikishwaji wa wananchi, siyo katika kupiga tu kura.

"Bali wanatakiwa kupata elimu pana kuhusu misingi ya katiba ya nchi, mgawanyo wa madaraka ya dola, haki ya wananchi na misingi mbalinbali ikiwamo haki ya kuishi, kutoa maoni, usawa mbele ya sheria," anasema.

Anaelezea pia wajibu na haki ya vyama vya siasa, namna ya kujilinda, uzalendo na wajibu wa wananchi kwa uongozi wa nchi na umuhimu wao wa kupewa elimu kuhusu sera na utayarishwaji wake.

### UTAWALA SHERIA

Anaendelea kueleza kuwa utawala wa sheria unahusu watu kutawaliwa na sheria, watu wote ni sawa katika sheria, ila watenganishwa na mamlaka ya serikali kuu, bunge na mahakama. "Jaji Samatta anasema, lengo la kutenganisha mamlaka ya serikali kuu, bunge na mahakama na jamii kwa ujumla, ni kuruhusu kudhibitiana, lakini pia mamlaka hizo ziwajibike kwa katiba," anasema.

Judith anasema, vinginevyo wananchi watabaki wanalia wakitafuta haki wakati mamlaka hizo ziko kimya, na kwamba uwajibikaji wa sheria ni moja ya misingi ya utawala wa sheria, unaojumuisha utunzaji wa sheria unaokubalika, na ulio wazi unaofanywa na vyombo hivyo.

Anazidi kuelezea kile ambacho Jaji Samatta amekiandika katika kitabu chake kuwa anagusia jeshi la polisi kufanya kazi kwa weledi na kujiepusha na rushwa na upendeleo kwa kufuata misingi ya sheria.

"Mwandishi anasema vikwazo dhidi ya utawala bora ni kutojibika kuwajibika kiutendaji, kimaadili na pia utaalam wa utendaji bora, unaotokana na ukosefu wa elimu, lakini pia woga nje na ndani ya serikali, hivyo, ili kuepuka hilo, ni muhimu kusema ukweli," anasema.

Anaendelea kuelezea kilichoandikwa kuwa Jaji huyo analigusa bunge kwamba linapokwama kuwajibika ipasavyo, ni kikwazo kwa utawala wa sheria, na kwamba linatakiwa liisimamie na kuishauri serikali.

### SABABU ZA KITABU

Jaji Samatta anasema amekiandika kwa kuwa anatamani kuona haki inatendeka katika kila nyanja ili kuimarisha utawala bora unaoendeshwa kwa mujibu wa sheria akisema hauwezi kuwa tu falsafa, kila kiongozi awe wa serikali lazima awajibike kikamilifu kusimamia utawala bora,, kwani ili kufanikisha utawala bora, utendaji haki ni muhimu kwenye ofisi za tume ya uchaguzi na vituo vya kupigia kura na pia ni muhimu kuwapo haki kwenye mabunge na taasisi za kutunga sheria," anasema Jaji Samatta.

Anafafanua kuwa haki pia inatakiwa kuwapo katika ofisi za serikali kuu na taasisi zake, ndani ofisi za serikali za mitaa, vyombo vya utoaji haki na haki ya wananchi kulindwa dhidi ya uonevu na pia uovu na rushwa.

"Lakini pia haki ya wananchi kuheshimiwa na uongozi wa nchi yao, haki yao ya kushirikishwa katika maamuzi mbalimbali yanayohusu nchi yao. Matamanio yangu ni kutaka kuona yaliyomo katika kitabu changu yanaendelezwa, ili yatoe mchango kwa maendeleo ya nchi," anasema.

## Wanawake wasijidogoshe wanaweza adui yao ni mpinga maendeleo

**INATOKA UK. 11**

"Wanawake tunaweza tusijidogoshe. Sisi ni watu muhimu ila tukumbuke suala la usawa ni la mahusiano yenye kuleta maendeleo kila jinsi yaani KE na ME, sisi hatuvunji heshima ya ME tunachotaka ni haki, usawa na fursa sawa kwa kila jinsi".

Anakumbusha kuwa adui wa mwanamke siyo mwanamke kama wengi wanavyodai bali adui ni mwanaume asiyependa maendeleo wala usawa wa kijinsia, haki na fursa sawa kwa kila mmoja.

Waziri anasisitiza umuhimu wa kuandika na kuacha historia za kazi za wanawake wana mapinduzi na mashujaa waliofanya na wanaofanya mambo makubwa kwa taifa mfano , Bibi Titi, Sofia Kawawa, Biubwa Amour Zahor, mwanamapinduzi wa Zanzibar na harakati zao za kukomboa na kushirikisha wanawake kwenye siasa na kufikia usawa.

"Andikeni historia zenu na za waasisi wa TAMWA, mwandikeni Rais Samia na nyingine za watu mbalimbali ili zifahamike ….." Anasema.

Anazungumzia suala la mafunzo na umuhimu wa kuwafundisha wanawake na wanahabari masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHEMA) na matumizi ya teknolojia za kielektroniki katika kazi mbalimbali ili kufikia mafanikio maana wanawake bado wako nyuma.

Anasema kozi za mafunzo ya TEHEMA na masuala ya kielekitroniki ni muhimu ili kuingia kwenye 'board room' na kuchambua mambo akisema ni lazima kufunza wanawake wengi ili wawe sehemu ya menejimenti.


"Wanawake wengi wanaweza uongozi, wakipewa mafunzo haya watamudu zaidi nisema kuwa hilo limethibitishwa kuwa mashirika, kampuni na taasisi zinazoongozwa na wanawake zinakuwa na mafanikio zaidi," anasisitiza.

Wito wa Waziri kwa TAMWA ukawa kuongeza juhudi kusaidia kudhibiti mmomonyoko wa maadili ili kuwa na taifa lenye muelekeo mwema na linaloheshimu na kuwa na hofu ya Mungu.

Na Mwandishi Wetu

# Mabadiliko tabianchi Dubai yanapoanza na mguu mzuri

## • Ni utayari 'fuko' la kufidia madhara



Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, António Guterres (kushoto), Rais Samia Suluhu Hassan na Mwenyekiti wa COP 28, Dk. Sultan al-Jaber. **PICHA: IKULU**

MKUTANO wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28), unaendelea jijini Dubai Falme za Kiarabu, safari hii unaelezwa kuwa umeanza na mambo mazuri.

Ni baada ya wajumbe wa mkutano huo kuridhia kuanzishwa kwa mfuko uliokuwa unaongojewa kuundwa kwa muda mrefu wa kulipa fidia ya madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabia nchi, yanayosababishwa na majanga kama mvua zenye madhara na ukame.

Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na viongozi mbalimbali duniani, wameuhutubia mkutano huo, unawakutanisha wajumbe wa mataifa takriban 200 duniani, wakiwamo wakuu wa nchi, viongozi wa taasisi za kifedha na biashara, wawakilishi wa mashirika ya serikali pamoja na asasi za kiraia, unamalizika sasa ukiwa umeanza tangu Novemba 30, ukitarajiwa kuhitimishwa Desemba 12, 2023.

La kufurahisha, wajumbe wa mkutano huo wameridhia kuanzishwa kwa mfuko uliokuwa unaongojewa kuundwa kwa muda mrefu wa kulipa fidia ya madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabia nchi, yanayosababishwa na majnga kama mvua zenye madhara na ukame.

Kwa kawaida makubaliano kama hayo hufikiwa katika dakika za mwisho wa mkutano huo baada ya siku kadhaa za majadiliano makali na kukwaruzana, lakini cha kustajabisha safari hii makubaliano yamefikiwa katika siku ya kwanza ya COP28, inasema BBC.

Rais wa COP28 Sultan al-Jaber anaushangaza mkutano huo katika siku ya kwanza kwa kutambulisha uamuzi wa kuanzishwa kwa mfuko huo muhimu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, mbele ya wajumbe wa mkutano huo na kupokelewa vizuri. Katika kuitikia wito wa kuanzishwa kwa mkutano huo Umoja wa Ulaya, Uingereza na Marekani pamoja na mataifa mengine mara moja walitangaza kuchangia kiasi kinachofikia dola za Marekani milioni 400, kwa mataifa masikini yanayokabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Kwa miezi 12 mataifa mbalimbali yalikuwa kwenye majadiliano ya taratibu za mfuko huo na utakuwa wapi pamoja na nani hasa anapaswa kulipwa fidia. Makubaliano kamili yalifikiwa wiki kadhaa kabla ya kukutana Dubai, inasema BBC.

Mara baada ya kuafikiwa kuanzishwa kwa Mfuko wa Kulipa Fidia ya Madhara ya Tabianchi, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) unaahidi kutoa dola milioni 100, Ujerumani milioni 100, Marekani yenyewe inaahidi dola milioni 17, iwapo itafikia makubaliano kwenye mkutano huo.

### TANZANIA NA COP28

Ujumbe wa Tanzania COP28 unaoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, uliwashirikisha mawaziri, makatibu wakuu, mabalozi, viongozi na wataalam kutoka wizara za kisekta, idara za serikali, mashirika ya umma, vyuo vikuu, sekta binafsi, asasi za kiraia, vijana na wanahabari kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Wakuu wa nchi na serikali wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi wamehutubia mkutano huo na Rais Samia ni mzungumzaji wa 11 miongoni mwa wakuu wa nchi na serikali takribani 160 wanaoshiriki.

Katika hutuba yake Rais Samia anayataka mataifa duniani kutambua kuwa suluhisho la uhakika la kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ni kutimiza ahadi za kutoa fedha na kuongeza kasi ya mikakati ya kudhibiti janga hilo.

Aidha, anakumbusha kuwa ilitolewa ahadi ya dola za Marekani bilioni 100 kila mwaka ili kukabiliana na mabadiliko katika mkutano wa Copenhagen na ahadi hiyo haijatekelezwa licha ya kiasi hicho kuwa kidogo kuliko kilichohitajika.

Rais Samia anasema mkutano wa Paris Ufaransa uliazimia kudhibiti ongezeko la joto chini ya nyuzi joto 1.5, lakini hali ni kinyume kwani kasi ya ongezeko la joto kwa sasa duniani inatia wasiwasi.

Aidha, anasema kushindwa kutimiza ahadi kunapunguza mshikamano na imani na kuleta matokeo mabaya kwa nchi zinazoendelea, ikiwamo Tanzania, ambayo hupoteza kati ya asilimia 2.0 hadi 3.0 ya pato la taifa (GDP) kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa zinazidi kukosa matumaini.

Pamoja na Rais Samia kuhutubia mkutano huo, Tanzania inaandaa na kuwa mwenyeji wa mikutano mikuu mitatu ya pembezoni, inayohusisha nishati safi ya kupikia, kilimo endelevu na uchumi wa buluu.

Rais Samia ndiye anayewaongoza viongozi wa nchi mbalimbali na taasisi za kimataifa kuzindua Programu ya Kuwakomboa Wanawake wa Afrika Kupitia Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (Africa Women Clean Cooking Support Programme(AWCCSP).

Katika uzinduzi wa mradi huo unaokusudia kuleta mageuzi na kumkomboa mwanamke, Rais Samia anatumia dakika 15 kuyashawishi mataifa ya Afrika kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mradi huo, kazi aliyoifanya Jumamosi iliyopita ikiwa ni sehemu ya shughuli za COP28 huko Dubai.

Katika uzinduzi huo, washiriki walitazama video iliyohesabu kutoka tisa hadi moja na kisha likaonekana jiko la gesi lenye herufi za AWCCSP, ambacho ni kifupi cha jina la mradi huo, ambao Rais Samia amezindua ngazi ya Afrika, baaada ya kuanza utekelezaji wa Dira ya miaka 10 inayokusudia kuongeza matumizi ya nishati safi za kupikia kwa asilimia 80 ya Watanzania.

Programu hiyo inalenga kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kukabiliana na changamoto za afya, mazingira, uchumi na kijamii ambazo huathiri zaidi wanawake na watoto, kutokana na ukweli kuwa kinamama hutumia muda mrefu kusaka kuni, hivyo programu hiyo itawapa muda wa kutosha kushiriki shughuli za maendeleo.

### MATARAJIO COP28

Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, kinaeleza matarajio ya Tanzania kwenye mkutano wa COP28 ni pamoja na kuhakikisha msimamo wa nchi unakubaliwa kwa kupata fursa za kupata fedha, kuwezesha miradi ya pamoja na teknolojia za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Tanzania inaunga mkono hoja ya kuongeza fedha za ufadhili kwa kuzingatia athari zinazozidi kuongezeka kwa sasa na kuhakikisha ahadi ya nchi zilizoendelea kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi zinatimizwa.

> Pamoja na Rais Samia kuhutubia mkutano huo, Tanzania inaandaa na kuwa mwenyeji wa mikutano mikuu mitatu ya pembezoni, inayohusisha nishati safi ya kupikia, kilimo endelevu na uchumi wa buluu.

Aidha, inasema ni kuhakikisha mkutano unaridhia uanzishwaji wa mfuko wa kupambana na majanga na maafa yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha juhudi za kuelekea matumizi ya nishati safi zinakuwa jumuishi na kujikita pia katika nishati safi za kupikia kwa kina mama vijijini kama njia ya kuhimiza nishati za mpito zinazozingatia usawa wa kijinsia.

Kuhakikisha mjadala wa masuala ya jinsia unazingatia maadili ya kitaifa na kijamii na wanawake wanapewa kipaumbele katika hatua za kushughulikia mabadiliko ya tabia nchi.

### UMUHIMU CO28

Mkutano wa COP28 unatarajiwa kuhuisha lengo la muda mrefu la dunia la kudhibiti ongezeko la joto kwa kiwango cha nyuzi joto 1.5. Mataifa takriban 200 yaliafikiana hatua hiyo jijini Paris 2015. Lengo la kiwango cha nyuzi joyo 1.5 ni muhimu ili kuepusha madhara na maafa ya mabadiliko ya tabianchi, kwa mujibu wa chombo cha Umoja wa Mataifa cha Hali ya Hewa (IPCC).

Viwango vya sasa vya ongezeko la joto vinavyokubalika ni kati ya nyuzi joto 1.1 ama 1.2, ukilinganisha na kipindi ambacho hakukuwa na viwanda.Hata hivyo katika siku za hivi karibuni, dunia inakaribia kufikia ongezeko la joto la nyuzijoto 2.4 hadi 2.7 ifikapo 2100, ingawa takwimu sahihi hazina uthibitisho.

Kaulimbiu ya COP28 ni "Umoja, Tekeleza, Fanikisha", wakati kaulimbiu ya Tanzania kwenye COP28 ni "Kuimarisha Kilimo Himilivu na Uchumi wa Buluu katika kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi".

JUKWAA LA VIONGOZI

UJIO SOMALIA EAC

# Haya ni muhimu; mosi mwanachama kulipa ada, jumuiya kujitegemea

• Ijitafakari ina miaka 23 bado inaomba wafadhili

**Na Christina Mwakangale**

SOMALIA inakuwa nchi ya nane ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ikiungana na waanzilishi wa Jumuiya hiyo, Tanzania, Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi, Sudan Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Ni taifa ambalo halijatengamaa kisiasa tangu kuondolewa kwa kiongozi aliyekuwa na mtizamo wa kupendelea mrengo wa kijamaa Mohammed Siad Barre, ofisa wa jeshi aliyeiongoza nchi hiyo kuanzia 1969 hadi Januari 1991

Deus Kibamba, mhadhiri Chuo cha Diplomasia jijini Dar es Salaam, anapozungumzia ujio wa Somalia EAC, anasema ni wakati sasa kufanyia maboresho mkataba wa jumuiya unaoruhusu kuongeza wanachama wapya, akiongeza kuwa vipo vipengele kadhaa vya Mkataba wa EAC, ambavyo vinahitaji maboresho kama vile kigezo cha mwanachama kulipa michango kwa wakati.

"Kigezo kiwe mwanachama alipe ada au awe na uwezo wa kujilipia mwenyewe, kuna nchi mbili hazilipa michango kwa miaka miwili. Napendekeza mwanachama alipe ada kwa wakati, ili kuifanya jumuiya ijiendeshe na kujitegeme.Pia EAC kwa kuwa inakua, iandae bajeti ambayo wanachama wanamudu kuiwezesha, kwa sababu karibu asilimia 80 ya bajeti inawategemea wahisani ambao awali walikuwa wakoloni wa nchi wanachama," anasema Kibamba.

"Wamepitisha bajeti takribani Shilingi bilioni 250 ambayo kwa kiwango kikubwa inatoka kwa wafadhili hivyo vigezo vya kujiunga vinahitaji maboresho hasa namna ya kupata fedha kwa njia endelevu.Nasema liwepo angalizo kwa wanachama wanaotaka kujiunga kwa kuwa baadhi hawajaimarika kiusalama, hivyo inaweza kuchangia nchi zingine kuingia katika migogoro hata vita." anaonya

Anapendekeza, wananchi wapewe uwanja kutoa maoni na yafikishwe kwenye jumuiya, ili kuboresha umoja huo, akisema baadhi ya wananchi wanaona EAC ni ya viongozi pekee.

"Hata namna wabunge wa EAC wanavyopatikana, kwa mfano wawakilishi wa bunge hilo kutoka Tanzania, wanapitishwa na wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huko Dodoma. Hoja kwa wananchi ni kwamba iwepo fursa wenyewe kuwapata wabunge hao na si kama ilivyo sasa wanapopatikana kutoka wabunge ambao pia nao wamechaguliwa na wananchi," anasema Kibamba.

Kipindi cha Meza ya Duara kinachotangazwa na DW, kinawakutanisha wachambuzi wa kisiasa wa ukanda wa Afrika Mashariki, wenye maoni na mitazamo tofauti kuhusu makaribisho ya Somalia EAC hivi karibuni, mjadala ambao gazeti hili linaufuatilia.

Katika majadiliano hayo, Dk. Abdullah Makame, mbunge Bunge la Afrika Mashariki (EALA), kutoka Tanzania, anasema zipo fursa za maendeleo na kiuchumi zilizotazamwa na wanachama kabla ya kukaribisha mgeni.

"Bila shaka waheshimiwa wa nchi wameangalia vigezo kwamba Jamhuri ya Somalia, kupitia EAC inaweza kupata fursa. Kwanza viongozi hawa wameondoa mipaka ya ramani ambayo tumeirithi kutoka kwa mkoloni".

Hata hivyo anasisitiza kujenga uelewa miongoni mwa wananchi katika jumuiya hiyo, ili kukuza ufahamu na manufaa ya EAC na kwamba wanahitaji kushirikiana kadri nafasi zinaporuhusu, ila kama Bunge la Jumuiya wanatamani kuwafikia wananchi hadi ngazi za mashina kuwaelewesha kuhusu jumuiya hiyo.

Makame anaongeza kuwa utaratibu wa kulinda usalama hutegemewa kwa nchi zote wanachama, akisema vitisho vilikuwa vikubwa awali, lakini sasa vimepungua na Somalia inaonekana imetulia, hivyo ilistahili kujumuishwa.

"Mwambao wa Somalia una kilomita 3,000 ni wazi utafungua biashara katika bandari zetu, unategemewa kuleta ushindani katika ukanda wa Afrika kwa kuungana na si kubakia vipande vipande. Tunataka kufungamanisha uchumi wa jumuiya kwa pamoja."

Anasema baadhi ya wanachama wapo kwenye jumuiya nyingi lakini wanachotaka ni kufungamanisha uchumi, akitoa mfano wa Jumuiyaya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini mwa Afrika COMESA na EAC, lakini hakuna maendeleo na ni hali ambayo imeathiri sana eneo letu."

"Tujue malengo ya mtangamani ni nini? Watu wapige kura kuchagua viongozi wao, kujivunia utengamano wa jumuiya, najivunia dhamira ya mkataba wetu, idadi kubwa ya nchi zetu ni vijana. Hawako tayari kuvumilia urasimu," anaonya Dk. Makame.

"Itifaki ya umoja wa forodha, panahitajika kamati ya biashara kusimamia shughuli zetu, imepita miaka 18 katika EAC lakini hakuna mwafaka, vijana wanakuja na ndio wengi Afrika hawatakuwa tayari kuvumilia haya," anaonya Makame.

Maimuna Mwidau, msomi kutoka Mombasa Kenya, ni mchangiaji wa Meza ya Duara, anayesema Somalia kujumishwa EAC kumezingatiwa suala la kisiasa, akisema karibu nusu ya Wasomali wapo Kenya, ni vigezo vya kisiasa vimetumika. Zaidi, pia Kenya inafanya biashara na Somalia, ni fursa kwa soko la EAC na Wakenya watanufaika, ila Somalia itafaidika zaidi.

Maimuna anazungumzia baadhi ya mogogoro katika ya Kenya na Somalia hasa katika mipaka, akisema pengine ni wakati mwafaka kwa Somali kufahamu namna ya kuishi ndani ya EAC akisema tatizo kubwa ni kukosa usalama, linalotiliwa shaka na wengi, Somalia kuwa katika EAC pengine itasaidia kuondoa mipaka, kwamba sisi sote ni ndugu.

Anaona hatua ya Somalia, kuingia EAC ni ya kubadili tabia na mtazamo wa Wasomali, kwamba wote ni ndugu jambo ambalo litaimarisha umoja miongoni mwao.

"Nchi za EAC bado ni maskini zinajitahidi kujikwamua, lakini zimejitahidi kulinda usalama wa watu, na wana jumuiya hii, pia wakarimu, ikiwa soko litafunguka na faida kwa kila nchi, itafaa. Tusaidiane, ili kwa pamoja tufike tunapatamani," anasema Maimuna.

Kadhalika, mwandishi na mchambuzi wa masuala ya kisiasa na kiuchumi, kutoka Kampala ini Uganda, Ali Mutasa, anasema watu wengi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki bado hawajafahamu manufaa ya umoja huo, pengine wafanyabiashara pekee hunufaika.

"Watu wa kawaida hawahisi kwamba huu muungano ukoje, wanaona ni mtangamano baina ya viongozi. Ila kuna moyo wa wanachama kuwekeza Somalia, sasa matumani yatakuja kwa kwenda kuwekeza. Takwimu ziliwahi kutoka zikisema Somalia inaongoza kwa rushwa, lakini kuna baadhi ya maeneo yalitawaliwa na makoloni tofauti, bado wanatoauti hadi leo, itapita hata miaka 50 ili wawe sawa na kuwa taifa lililoendelea. Ila lazima nchi ianze ."

Kuhusu usalama, anasema inahitaji Somalia kuondoa vita vya wao kwa wao kutokana na ukabila, akisema taifa haliwezi kutengwa kwa hilo, bali wajumuishwe ili kujifunza.

Tumaini Munale, mkufunzi wa Chuo cha Ualimu Bunda mkoani Mara, mchambuzi wa masuala ya kisiasa na kijamii, anasema Somalia ilitamani kuingia EAC tangu 2012 huku wakijitahidi kupunguza changamoto zao, ambazo ni ukosefu wa utawala bora, uvunjifu wa haki za binadamu, amani duni na mashambulizi ya Al shabab.

"Wamesubiri kwa takribani miaka 11 hadi kukubaliwa.Ukiangalia DRC, Sudan Kusini bado nao wana changamoto kama hizo lakini wamekubaliwa, kwa nini Somalia, naona wameona wamepunguza kwa kiwango kikubwa. Ingawa bado haijapunguza kwa asilimia kubwa ila angalau wana vigezo wamepiga hatua na hata uchaguzi walifanya pamoja na wengi hawakushiriki, ila wamejitahidi," anasema Tumaini.

Anasema wasiwasi wa kiusalama haukwepeki ila tija itakuwa kubwa kwa kuongezeka kwa kiwango cha amani eneo la Pembe ya Afrika na kwamba Somalia atakuwa mnunuzi mkubwa wa mazao, na atapunguza kiwango cha ukabila, akikumbusha pia ipo katika Mamlaka ya Maendeleo ya Kiserikali (IGAD) ambayo Kenya ni mwachama .

"Kwa namna ilivyo sasa, tunaona jumuiya inazidi kukua na changamoto ndivyo zinaongezeka zaidi, mfano Jumuiya ya Kiuchumiya Mataifa ya Afrika Magharibi (ECOWAS) ina nchi 14, lakini bado kuna mapinduzi. Hivyo tunahitaji kuuondoa udhaifu wetu sisi wenyewe," anaongeza.



Rais wa Somalia, Hassan Sheikh Mohamud. PICHA: DW

> Itifaki ya umoja wa forodha, panahitajika kamati ya biashara kusimamia shughuli zetu, imepita miaka 18 katika EAC lakini hakuna mwafaka, vijana wanakuja na ndio wengi Afrika hawatakuwa tayari kuvumilia haya.



# Rushwa yakwamisha uwajibikaji serikalini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Pindi Chana, amesema uwapo wa vitendo vya rushwa nchini unaifanya serikali kushindwa kutekeleza ipasavyo jukumu lake la kuwahudumia wananchi.

Alisema hali hiyo inasababisha miradi ya maendeleo kutekelezwa chini ya kiwango kutokana na fedha zinazotengwa kuingia katika mikono ya watu wachache.

Akizungumza wakati akizindua maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu juzi jijini humo, Dk. Chana alisema serikali kupitia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Ruhwa nchini (TAKUKURU) imekuwa ikifanya ufuatiliaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ili kukabiliana na ubadhirifu ikiwamo rushwa.

"Serikali yetu imekuwa ikifanya juhudi kubwa, kudhibiti rushwa nchini na ninyi nyote ni mashahidi kwa kuwa mlimsikia Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, akiielekeza TAKUKURU kufanya ufuatiliaji katika miradi mbalimbali ya maendeleo ili kukabiliana na ubadhirifu ikiwamo rushwa.

Alisema vita ya rushwa nchini bado ni kubwa na vielekeza vyombo vya habari kutumia vizuri kalamu zao kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kushiriki kwa vitendo katika kukataa na kufichua vitendo hivyo ili kumaliza kabisa vitendo hivyo ambavyo ni kinyume cha sheria.

Kwa mujibu wa Dk. Chanda, maadhimisho ya mwaka huu yanaenda sambamba na ya miaka 75 ya tamko la Haki za Binadamu ambalo tangu kutangazwa kwake Desemba 10 , 1948 limeweka msingi wa mikataba mingine ya haki za binadamu.

Aidha, alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zimeliweka tamko hili katika katiba zao ambapo Tanzania ni ibara ya tisa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema ibara hiyo inaeleza mamlaka ya nchi na vyombo vyake vyote viwajibike kuelekeza sera na shughuli zake zote katika lengo la kuhakikisha kwamba heshima ya binadamu inahifadhiwa na kudumishwa kwa kufuata Kanuni za Tangazo la Dunia kuhusu haki za binadamu.

"Tunapoadhimisha Siku hii muhimu ya Maadili na Haki za Binadamu ni jambo muhimu tukumbuke kuwa tunapaswa kutekeleza wajibu wetu kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa na hivyo kuepuka kuathiri haki za binadamu kwa kushiriki rushwa.

"Wakati mwingine haki hizi za binadamu huathiriwa na tabia za baadhi ya watendaji wasio waadilifu ambapo rushwa huwa kigezo cha mtu kupata haki ya msingi," alisema.

Akitoa taarifa kuhusu shughuli mbalimbali zitakazofanyika kuelekea kilele cha maadhimisho hayo, Mkurugenzi wa Elimu kwa Umma TAKUKURU, makao makuu Joseph Mwaiswelo alisema kutakuwa na jukwaa la kitaifa la wadau ambapo mada maalum itawasilishwa na kujadiliwa.

Alisema ni matarajio kuwa jukwaa hilo litachangia kuimarisha misingi ya uwajibikaji na uadilifu katika sekta ya umma na sekta binafsi kwa ajili ya maendeleo endelevu ya taifa.



Wakazi wa Jiji la Dodoma wakiwatumia wanyama aina ya ng'ombe kama nyenzo ya usafiri, kwa kuvuta mkokoteni wenye mizigo katika barabara ya mji wa serikali Mtumba jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bashungwa aagiza usanifu daraja Munguri uharakishwe

**Na Paul Mabeja,** KONDOA

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amemwelekeza Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Dodoma kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa daraja la Munguri lililoko katika Mto Bubu wilayani Kondoa mkoani hapa ili gharama zake ziwekwe kwenye bajeti ya mwaka ujao.

Bashungwa ameyasema hayo juzi alipokagua eneo la daraja hilo linalokatisha barabara ya Kondoa, Mtiriangwi/Gisanbang inayounganisha mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara.

"Nitumie nafasi hii kumwelekeza Meneja wa TANROAD, mkoa wa Dodoma, usanifu wa daraja hili ufanyike mapema na inapofika wiki ya kwanza ya Januari 2024 nipate ripoti ili gharama za ujenzi ziwekwe kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24," alisema Bashungwa.

Aidha, Waziri Bashungwa alisema ujenzi wa daraja hilo ni muhimu kwa kuwa likikamilika litaunganisha mikoa mitatu ambayo mvua zinaponyesha wananchi wanakosa mawasiliano kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

Waziri Bashungwa alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuboresha miundombinu nchini hasa Mkoa wa Dodoma ambapo kuna miradi mingi inaendelea kutekelezwa.

"Kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais ameniagiza nifike hapa na niangalie vipaumbele na kufanya upembuzi yakinifu kwa kujenga daraja la kudumu katika wilaya ya Kondoa," alisisitiza Bashungwa.

Mbunge wa Kondoa Vijijini ambaye ni Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji aliomba serikali kupitia kuharakisha kujenga daraja hilo kwakuwa limekuwa kikwazo wakati wa mvua.

"Daraja hili ni muhimu kwa wakazi wa Kondoa, Manyara na Singida kwa ujumla kwa sababu ni kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi na pia ni daraja tegemezi wilayani hapa kwa usafiri na usafirishaji," alisema Dk. Kijaji.

Awali, akitoa taarifa kuhusu daraja hilo, Meneja wa Mkoa wa TANROADS, Dodoma Mhandisi Leonard Chimagu, alisema upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo unatekelezwa na serikali kwa kutumia fedha za ndani.

Alisema Mhandisi Mshauri wa mradi huo ni Crown- Tech Consult Ltd kwa gharama ya milioni 480.8 na fedha ya utekelezaji wa kazi hiyo umetengwa katika mwaka huu wa fedha.

Hata hivyo, alisema kukamilika kwa daraja hili kutaleta faida mbalimbali za kiuchumi katika mkoa wa Dodoma, Singida na Manyara.

## Mazao kuuzwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SERIKALI ya Mkoa wa Singida imesema kuanzia msimu wa kilimo ujao mazao ya alizeti, korosho, dengu na choroko na mengine yatauzwa kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani ili wakulima waweze kunufaika zaidi na hivyo kukuza uchumi wao.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba alisema hayo jana wakati akizungumza na watendaji wa kata, vijiji na maofisa ugani wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida kuwaeleza mkakati wa kuongeza maeneo ya kilimo katika msimu huu wa 2023/2024.

Alisema serikali itatumia mfumo wa stakabadhi ghalani ambao mazao hukusanywa pamoja kwenye ghala maalum lililosajiliwa na serikali kwa lengo la kuyauza kwa bei ya ushindani ili wakulima waweze kunufaika na kilimo.

Serukamba alisema inapofika msimu wa mavuno kumekuwa na wimbi la walanguzi kuvamia vijijini na kununua mazao kwa wakulima kwa bei ndogo ambayo haimnufaishi mkulima, suluhisho lake ni kuuza mazao kwa kutumia mfumo huo.

Mkuu huyo wa Mkoa aliwaagiza watendaji hao na maofisa kilimo kuwahamasisha wananchi hususani vijana wajishughulishe na kilimo cha mazao ya biashara na chakula hususani zao la alizeti ili kuongeza uzalishaji hilo kutoka asilimia 50 msimu uliopita hadi kufikia asilimia 70 msimu huu (2023/24).

"Sitanii, nataka tujiandae kusimamia kilimo, suala la watu kwenda shambani ni la lazima sio hiari, watu wote waende wakalime, tukifanya hivyo tutapata mavuno yatakayoondoa changamoto ya umaskini kwa watu wetu... tunataka Mkoa wa Singida uingie kwenye historia ya kuzalisha mafuta ya alizeti ili Taifa litutegemee kwa mafuta ya kula," alisema.

Aidha, Serukamba alisema katika msimu wa kilimo uliopita katika zao la alizeti Mkoa wa Singida ulichangia asilimia 50 ya zao hilo lililozalishwa nchini na kwamba malengo ya mwaka huu ni kufikia asilimia 70 kiwango ambacho kitafikiwa iwapo wakulima wataongeza nguvu katika kilimo.

**Alisema serikali itatumia mfumo wa stakabadhi ghalani ambao mazao hukusanywa pamoja kwenye ghala maalum lililosajiliwa na serikali kwa lengo la kuyauza kwa bei ya ushindani ili wakulima waweze kunufaika na kilimo.**





# RC asisitiza ubunifu kampuni za mbolea

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

KAMPUNI za mbolea zimetakiwa kuongeza ubunifu katika uzalishaji ili zipatikane kwa kwa urahisi na kuleta unafuu wa bei kwa wakulima nchini.

Rai hiyo ilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, wakati akifunga mkutano wa wadau wa kilimo Nyanda za Juu Kusini ulioandaliwa na kampuni ya kuzalisha mbolea ya Intracom uliofanyika mkoani hapa.

Mtaka alisema kampuni za uzalishaji wa mbolea inatakiwa kurahisisha upatikanaji wa mbolea ili wakulima waweze kupata kwa wakati na kufanya shughuli zao za kilimo.

"Kama mbolea zinalalamikiwa kwenda kwa wakulima wakati mvua zimeshanyesha wanatakiwa kuja na suluhu ya kupeleka mbolea kabla ya mvua kunyesha," alisema Mtaka.

Alizielekeza kampuni hizo kwenda na wakati kwa kuzingatia mahitaji ya wakulima kama vile kufikisha mbolea kwenye maeneo ya watu kabla ya msimu wa kilimo kuanza.

Aidha, alisema serikali ya awamu ya sita imefanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya kilimo kuhakikisha nchi inakuwa na uwezo kwa kuuza mazao ndani na katika nchi nyingine zilizopo barani Afrika.

Aliitaka kampuni ya Intracom inayozalisha mbolea ya Fomi kushughulikia changamoto zinazoweza kujitokeza ili zisiathiri soko la mbolea la kiwanda hicho.

Mwenyekiti wa Bodi ya Kiwanda cha Mbolea cha Intracom, John Chiligati, alisema kabla ya ujenzi wa kiwanda hicho Tanzania ilikuwa inaagiza mbolea kutoka nje ya nchi lakini kufikia mwezi Machi mwakani kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani za mbolea milioni moja kwa mwaka.

"Mahitaji ya mbolea hapa nchini kwa mwaka hivi sasa ni kati ya tani 700,000 hadi 800,000, kwa hiyo mwakani mwezi Machi tutakuwa na kiwanda kinachozalisha mbolea tani 1,000,000 maana yake ni kuwa mahitaji ya ndani yatatosheleza na ziada itauzwa nje," alisema Chiligati.

Mmoja wa wakulima walioshiriki mkutano huo, Sarafina Mwani, alisema upatikanaji wa mbolea kwa wakati utawasaidia kufanya maandalizi ya kilimo kwa wakati na kupata mazao mengi kwa ajili ya chakula na kiasi kingine kuuza.

"Kwa kweli upatikanaji wa mbolea ni changamoto kwa sasa lakini ujio wa kiwanda hicho utatusaidia sana kwani tutapata mbolea kwa wakati," alisema Mwani.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, ACP Ally Wendo (kushoto), Mtaalamu wa Afya na Usalama Kazini wa Kampuni ya Vodacom Tanzania, Adamson Manya (wa pili kushoto) na Meneja Msaidizi wa Rasilimali Watu wa kampuni hiyo, Maria Clarera, wakimkabidhi vifaa vya usalama barabarani Mwalimu wa Shule ya Msingi Mwangaza, Marian Juma (kulia), wakati wa uzinduzi wa kampeni kuhusu usalama wa jamii inayolenga shule zilizoko kando ya barabara nchini, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi yataja chanzo cha ajali iliyoua wanne

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe limesema chanzo cha ajali mbili tofauti zilizoua watu wanne na kujeruhi watatu, wakiwamo askari wawili wa usalama barabarani ni madereva hao kutozingatia tahadhari za usalama barabarani.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi, Mahamoud Banga, alisema gari ndogo Toyota Sienta namba T815 DXV iliyokuwa inaendeshwa na mmoja wa askari hao iliipita gari nyingine kwenda upande wa pili bila ya kuchukua tahadhari.

Alisema ajali ya kwanza iliyohusisha askari ilitokea majira ya saa 12:20 asubuhi katika Kijiji cha Isoliwaya kilichopo Kata ya Wanging'ombe Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe barabara kuu ya kuelekea mkoani Mbeya.

Aliwataja askari waliofariki kwenye ajali hiyo kuwa ni WP-CPL 7866 Elizabia Kizale (35) mwenyeji wa Chunya mkoani Mbeya na H.1027-CPL Patrick Salehe (34) mwenyeji wa Lushoto mkoani Tanga.

"Chanzo cha ajali hiyo ni gari ndogo iliyokuwa ikiendeshwa na askari polisi kutochukua tahadhari wakati ikiipita gari nyingine ya kwenda upande wa pili jambo ambalo lilipelekea magari hayo kugongana," alisema.

Alisema dereva wa gari aina ya Sharpman alitoroka na jeshi hilo linaendelea na jitihada za kumtafuta kwa ajili ya taratibu zingine za mahojiano.

Wakati huo huo, alisema ajali nyingine ilitokea majira ya saa tatu asubuhi eneo la Igawilo Kata ya Kifanya Halmashauri ya Mji wa Njombe ambapo gari aina ya HOWO T 765 DNZ yenye tela namba T912 DTW iliigonga gari ndogo Toyota VXR T602 EEC, kusababisha vifo vya watu wawili na dereva wake alitoroka.

"Watu wawili waliokuwa kwenye gari ndogo walifariki wakiwa wanapatiwa matibabu kwenye hospitali ya mkoa inayofahamika kwa jina la Wikichi," alisema Banga.

Aliwataja waliofariki kwenye ajali hiyo kuwa ni Luno Kasmiri Nyika (43) mkazi wa Mbinga na Scholastica Kasmiri Nyika (35) ambaye ni mtendaji wa kijiji hiko wilaya ya Mbinga.

Kamanda Banga alisema majeruhi ambao wanaendelea kupata matibabu katika hospitali ya Kibena ni Oscar Mgovani (43) dereva wa gari ndogo na Faraja Nyika (17) mwanafunzi aliyemaliza kidato cha nne mwaka jana pamoja na utingo wa gari kubwa Tarick Mohamed (20) na hali zao zinaendelea vizuri.

Alitoa wito kwa magari yote kuchukua tahadhari wakati wanatumia barabara kwa kuhakikisha wanafuata sheria za usalama barabarani pamoja na alama zake.

Kamanda huyo alisema maeneo mengi ya mkoa huo yana miteremko mikali na miinuko hivyo madereva wanatakiwa kuwa makini ili kuepusha ajali ambazo zinaweza kuzuilika.

# Watoto 1,121 wanaishi kwenye mazingira magumu Makambako

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

IMEELEZWA kuwa jumla ya watoto 1,121 wanaishi katika mazingira hatarishi katika Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Mji wa Makambako, Masinde Masinde, wakati wa kikao cha uzinduzi wa jukwaa la wadau wa ustawi wa mtoto.

Masinde alisema katika watoto hao wamo yatima, wenye ulemavu, wanaokosa mahitaji ya msingi, waathirika wa matukio ya ukatili na wale wanaoishi na wazazi wenye ulemavu au wenye maambukizi ya virusi vya ukimwi na kusababisha wakose mahitaji yao ya msingi.

"Kati ya hao watoto 1,121, watoto 230 wanahitaji mahitaji ya shule, 110 ni wenye ulemavu ambao wanahitaji kiti mwendo na mafuta, 230 mahitaji ya kawaida ikiwamo chakula, nguo, viatu na taulo za kike.

"Watoto 430 wanahitaji bima za afya, 20 wanahitaji kupata makazi huku vitanda na mashuka na mablanketi 327 yakitakiwa ili kuwasaidia watoto ambao wanalala chini," alisema Masinde.

Alisema pia kuna baadhi ya kaya watoto wapo nyumbani hawana ujuzi wowote hivyo wanahitaji kupatiwa elimu ya ufundi stadi lakini kuna kaya 21 zinahitaji uwezeshaji wa kiuchumi.

Mratibu wa jukwaa hilo Mkoa wa Njombe, Erick Haule, alisema jamii inawajibu wa kuhakikisha inawasaidia watoto hao kupata mahitaji yao ili waweze kutimiza ndoto zao.

"Lengo haswa la jukwaa hili ni kuweza kutoa fursa kwa wadau mbalimbali kutoa michango yao kufadhili mahitaji mbalimbali ya watoto ambao wapo kwenye mazingira hatarishi," alisema Haule.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Apiya Mayemba, alisema ili watoto hao wapate mahitaji hayo ni lazima wadau mbalimbali hasa wananchi tajitoee kuwasaidia.

"Jambo hili ni letu sote tunakwenda kupunguza athari ndani ya jamii yetu kwa maana ya wale watoto kwa mahitaji yote yanayohitajika, tunatamani kila mtoto aweze kupata hitaji lake kama binadamu wengine," alisema Mayemba.

Baadhi ya wadau akiwamo mchungaji, Godlove Mtagawa alisema jamii inapaswa kuungana ili kuwawezesha watoto hao kupata mahitaji yao ambayo yatawasaidia kupata haki yao ya msingi ya kuendelezwa kielimu.



# Talaka chanzo wanawake kupata ugonjwa wa akili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

DAKTARI wa afya ya akili katika Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongo Chekundu, Khadija Abdulrahman Omar, amesema kuwa wimbi la takala linaathiri wanawake kupata changamoto ya afya ya akili baada ya ndoa kuvunjika kwa kupewa talaka.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya ujio wa jumuiya za wanawake wajane kutoka Afrika ikiwamo Nigeria, Ethiopia na Tanzania Bara na Zanzibar kutembelea hospitali hiyo na Tume ya Ukimwi na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Dk. Khadija alisema wanawake wengi wa Zanzibar katika ndoa huwategemea wanaume kwa sababu ndio wenye kipato na kulisha familia ikilinganishwa na wanawake hivyo ndoa ikivunjika au mume kufariki janga la malezi humwangukia mwanamke.

"Ukiachwa au mume kufariki janga lote la malezi la watoto humwangukia mwanamke hivyo hupelekea kupata msongo wa mawazo na kupata tatizo la afya ya akili," alisema.

Daktari huyo alisema kuna wimbi kubwa la wanawake wajane ambao ndoa zao zimevunjika kwa kupewa talaka wameathirika kiakili na hufika hospitalini hapo kwa ajili ya kupata tiba.

Aidha, alisema athari ya wimbi la talaka halipo kwa wanawake pekee hata kwa watoto nao hupata changamoto ya afya ya akili kwa sababu kabla ya talaka kutoka huwa kuna udhalilishaji ikiwamo ugomvi au wazazi kutoelewana ambavyo huwaathiri kisaikolojia.

"Hivi sasa pia tumekuwa na changamoto kubwa ya watoto wenye tatizo la afya ya akili ambao tunawapatia huduma ya matibabu hospitalini hapa, wazazi kutoelewana katika familia humwathiri mtoto kisaikolojia na wakati mwingine kukosa haki zake zinazotakiwa," alisema.

Alisema wastani hupokea wagonjwa wapya wa afya ya akili 150 katika hospitali hiyo wakiwamo wanawake wajane ambao ndoa zao zimevunjika aidha kwa kupewa talaka au mume kufariki.

Daktari huyo alisema ili kupunguza wimbi la takala ni vyema mafunzo ya ndoa yaboreshwe na kuhakikisha mafunzo hayo yanatolewa kwa watu wote wanaoingia katika ndoa na waliomo katika ndoa lakini wakati wa utoaji wa mafunzo hayo kuhusishwe wataalamu wa afya ya akili.

"Katika ndoa kuna changamoto za kihulka na hupelekea ugomvi katika ndoa lakini hulka hizo hazitambuliwi na anayeweza kugundua hilo ni wataalamu wa afya ya akili hivyo ni vyema katika utoaji wa mafunzo ya ndoa kushirikishwa na wataalamu wa afya ya akili," alisema.

Alisema kutokana na wimbi kubwa la wagonjwa wa afya ya akili kuna changamoto ya uhaba wa wataalamu wa afya ya akili na hulazimika mtaalamu mmoja kuhudumia wagonjwa 60 kwa siku.

Alisema serikali inaendelea kuchukua juhudi za kuwasomesha madaktari wa afya wa akili na tayari madaktari bingwa saba wameshárudi masomoni na wengine wanaendelea na masomo yao ikiwamo nje ya nchi.

Hata hivyo alisema licha ya kutoa tiba kwa wagonjwa wa afya ya akili lakini pia huwapa elimu ya ujasiriamali ili kupata kipato ambacho kitasaidia kuendesha maisha yao hasa kwa wale wanawake wajane ambao wamepata changamoto hiyo ya afya ya akili.

Mkurugenzi wa Jumuiya ya Wajane Zanzibar, Tabia Makame Muhammed, alisema kuna haja ya kukaa kwa pamoja katika kupunguza wimbi la talaka linaloleta athari kubwa katika jamii ikiwamo watoto kutelekezwa.

Mkurugenzi wa Tume ya UKIMWI Zanzibar, Dk. Ahmed Khatibu, alisema kuwa tafiti iliyofanyika Zanzibar miaka miwili iliyopita alisema zaidi wanawake wajane ndio wanaopata maambukizi ya Virusi vya Ukimwi ikilinganishwa na wanawake wengine.

"Kwa mfano tafiti tunayoifanya kila baada ya miaka miwili ya kuangalia maambukizi ya virusi vya VVU kwa mama wajawazito unakuta wengi wao wenye VVU ni wajane ikilinganishwa na wale ambao wamo katika ndoa au ambao hawajaolewa," alisema.

Aidha alisema maambukizi ya VVU yapo juu zaidi kwa wanawake wanaofanyabiashara ya ngono ambayo ni asilimia 21.1 lakini sababu kubwa ya kuingia katika biashara hiyo ni kuvunjika kwa ndoa na kuwa katika hali ya ujane.

"Wengi tuliowahoji wanaofanya biashara hii ni wajane aidha ameachika katika ndoa au mume wake kafariki na kuachiwa watoto bila ya msaada wowote hivyo hujiingiza huko ili kupata kipato cha kuendesha familia yake, " alisema.

Hata hivyo alisema mjamzito aliyekuwamo katika ndoa anapogundulika kuwa ana maambukizi ya VVU ndoa hiyo huvunjika kwa kupewa talaka hivyo tume hiyo inasisitiza wanapoenda kupima afya zao kwenda wa weza wao ili kupunguza wimbi la talaka kwa sababu wakati mwingine mwanamume ndiye mwenye maambukizi.

"Mmoja kati ya wanandoa akigundulika kuwa ana maambukizi ya VVU isiwe sababu ya ndoa kuvunjika kwa sababu upo uwezakano wa kuishi pamoja katika maisha yao ya ndoa kwa kufuata utaratibu kutoka kwa wataalamu wa afya, na Zanzibar hii wapo wanaoishi ambao mume ana VVU na mke hana maambukizi na wanafurahia maisha yao ya ndoa," alisema.



Daktari wa Afya ya Akili wa Hospitali ya Kidongo Chekundu Zanzibar, Khadija Abdulrahman Omar, akionyesha kwa waandishi wa habari jana baadhi ya bidhaa zinazotengenezwa na wagonjwa wa afya ya akili wanaofika hospitalini hapo. Wagonjwa hao baada ya kupatiwa matibabu pia hupewa elimu ya ujasiriamali. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Waziri aagiza wazazi kucheza na watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, amewaelekeza wazazi kuwa na utamaduni wa kucheza na watoto wao maana kucheza pamoja na watoto sio ushamba bali kunaongeza mapenzi na furaha.

Akizungumza katika mahafali ya pili ya Shule ya Iqram huko Mpendae nje ya mji wa Zanzibar, alisema jamii imekuwa na watu katili kwa watoto, baadhi yao ni sehemu ya familia au wa karibu lakini hawana nia njema na watoto.

Aliwataka walezi na wazazi kila mmoja kusimamia malezi ya mtoto wake ili kuwalinda na vitendo vya udhalilishaji ikiwamo ulawiti na ubakaji kwa sababu hali ni mbaya.

"Niwaombe wazazi wenzangu kila mmoja kusimamia malezi ya mtoto wake, kujali mtoto wako anafanya nini, yupo wapi, muda gani na huko aliko uhakikishe anacheza na nani na anayecheza naye anatabia gani kwa sababu kuna baadhi ya watoto wameshaathirika, wameshalawitiwa na kubakwa," alisema.

Alisema baadhi ya watoto waliolawitiwa na kubakwa na athari walizonazo wanazipeleka kwa watoto wenzao ambao hajaathirika na vitendo hivyo ni vyema kuchukua juhudi ya kuwalinda watoto wote.

Aidha, alisema kuwa udhalilishaji mkubwa unafanyika zaidi kwa watoto wenye ulemavu hivyo ni vyema kila mmoja kupinga vitendo hivyo viovu ambavyo vinaathiri kimwili, kiakili na kimaendeleo.

Mkurugenzi wa Shule hiyo, Khadija Said, alisema wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa kiwanja cha michezo hasa ikizingatiwa kuwa michezo ni afya kwa watoto.

"Mtoto bila ya kucheza hawezi kumaliza makuzi yake, ili ukuaji wake uwe mzuri apate elimu lakini pia ashiriki michezo," alisema mkurugenzi huyo.

Mbunge wa Jimbo la Mpendae, Taufiq Salum Turky, aliahidi kujenga viwanja vya michezo katika eneo lililopo karibu na shule hiyo ili watoto wote wa jimbo hilo kukitumia kiwanja hicho.

Aidha, alisema lazima jamii kuwajengea mazingira rafiki ya kupata elimu tokea ngazi ya chini na Rais wa Zanzibar Dk. Mwinyi anafanya jitihada za kujenga majengo ya shule ya kisasa ili elimu inayotolewa kuwa bora.

Alisema kushamiri kwa vitendo vya udhalilishaji kunachangiwa na kuporomoka kwa maadili hivyo ni vyema jamii kurudi katika maadili, tamaduni na kuwa na imani ya hofu ya Mungu kwa sababu vitendo hivyo vimepingwa na havikubaliki katika dini zote.

## Sheria mpya ya uwekezaji kuipandisha hadhi Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema sheria mpya ya uwekezaji Zanzibar itaifanya Zanzibar kuwa kituo bora cha uwekezaji duniani na kuwapo fursa nyingi za uwekezaji.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, wakati akiwasilisha marekebisho ya sheria mpya ya uwekezaji Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Alisema sheria ya uwekezaji ni bora na imeondoa urasimu na kuwafanya wawekezaji wenye nia ya kuwekeza kukamilisha utaratibu wa mambo yote katika kipindi kifupi.

Soraga alisema serikali imekuja na marekebisho ya sheria hiyo kwa lengo la kuongeza ufanisi na ushawishi wa uwekezaji kupitia taasisi mbalimbali za nje ya nchi.

"Kwa mfano sheria ya zamani ya Mamlaka ya Uwekezaji uchumi ZIPA haijaainisha uwekezaji wa mafuta na gesi katika sheria yake ya zamani," alisema.

Aidha alisema sheria hiyo pia haijataja uwekezaji wa kuelekea uchumi wa buluu pamoja na visiwa vidogo viliopo Unguja na Pemba ambapo serikali imetangaza uwekezaji wake.

"Sheria mpya ya uwekezaji imekuja na mambo mengi ambayo yanakwenda sambamba na sera ya uwekezaji na mikakati ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi katika uwekezaji ikiwamo kuondosha urasimu kwa uwekezaji kwa diaspora katika mambo ya msingi ikiwamo umiliki wa ardhi," alisema.

Naye Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Ali Suleiman Amneir, alisema sheria hiyo inakwenda sambamba na sheria za uwekezaji zilizopo katika nchi ambazo zinakwenda na kasi ya uwekezaji nchini.

Alisema sheria mpya ya uwekezaji iliyowasilishwa sasa inakwenda sambamba na sheria ziliopo katika nchi zilizopiga hatua kubwa ikiwamo Ghana na Ethiopia zenye idadi kubwa ya diaspora.

Mwakilishi wa Jimbo la Dimani Mwanaasha, Khamis Juma, alitaka sheria hiyo ilete mageuzi makubwa pamoja na kutoa fursa za ajira kwa wananchi wetu katika uwekezaji unaofanywa.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Mohamed Said, alisema mabadiliko ya sheria mpya ya uwekezaji sasa yatawezesha kuwapo kwa mpango wa ukodishaji wa visiwa vidogo viliopo Unguja na Pemba katika uwekezaji na hivyo kuzalisha ajira.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**JUDITH HOPE KIDENYA** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 010651** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam mwaka 2018. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/UBU/50177/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JULIETH JAPHET RUTAIHWA** anatangaza kupotelewa na Result slip ya kidato cha sita yenye index namba S.0489/0529 iliyotolewa na SUJI SEKONDARI mwaka 2023. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/34408/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SABRA FRANK PANDUKA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4554/0093** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia HENRY GOGARTY SEKONDARI mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/KAG/BIH/3231/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**DANIEL PHILLIPO SARWATT** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 776 BEL** aina ya TOYO. Chassis namba **KE7KEFPK032368.** Engine namba **162FMJPK032368.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/1428/2023.**

## KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**ANITA MARCO OLOTU** ANATANGAZA KUPOTELEWA KWA HATI YA OFA YA KIWANJA YENYE JINA LINA MARIALLE PLOT NAMBA **19 BLOCK E,** KILICHOPO WILAYA YA MOSHI KATA YA MAJENGO MTAA WA MSIKITINI. KWA YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KATIKA KITUO CHA CHOLOSI KILICHOPO KARIBU NAYE. TAARIFA YA POLISI **PHQ/KIL/MOS/471/2023**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA DISTRICT**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 26605 OF 2023**

**In the matter of the Estate of the late ABDILLAH SHABANI LACHA a.k.a MOSES S. LACHA of Dodoma City**

**AND**

**In the matter of application for the letters of administration by NDEMWILISA ELINISA LEMA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above-named deceased Person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above-named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 2 .............day of 1..................2024
Dated at Dodoma this 1st day of NOVEMBER 2023

Resident Magistrate

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**LA WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**

**MAOMBI MADOGO NA.523 YA MWAKA 2022**

**ALICE MSANGAA................................MSHINDA TUZO**

**VERSUS**

**JOHN SANGA................................MSHINDWA TUZO**

**KWA:**
**JOHN SANGA**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi,Wakili au Mwakilishi yoyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 19.01.2024 saa 3.00asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:** -Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu,Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito,Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 20 ya Mwezi wa NOVEMBA,2023.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 93/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ASHA ABDALLAH MWENGE wa DODOMA KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ABDALLAH MWENGE CHIPS**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19 Mwezi 12 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo Tarehe 01 Mwezi 12 Mwaka 2023.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 135 OF 2023**
**In the matter of the Estate of the late BERNADETA WILLIAM KITELANYA of Veyula within Dodoma Region**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY JUMANNE MAGANGA SESA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 163)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 13 Day of 12, 2023
Dated at Dodoma this 2nd Day of November, 2023.

RESIDENT MAGISTRATE

---


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.**



**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

**0745 700 710.**

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Israel kusababisha mafuriko Gaza

**JERUSALEM,** Israel

KWA mujibu wa ripoti ya 'Wall Street Journal' (WSJ) ambayo imewanukuu maofisa wa Marekani wakibainisha mpango wa Israel inayofikiria kusukuma maji ya bahari kwenye vichuguu vya Gaza ili kuwaondoa Hamas wanaodhaniwa kujificha kwenye mapango chini ya ardhi.

WSJ inabainisha kwamba Israel inaweza kutekeleza mpango huo kwa kutumia mtandao mkubwa wa pampu ambao unaweza kuingiza maelfu ya mita za ujazo za maji kwenye vichuguu, na kuzifurisha ndani ya wiki.

Inaeleza kuwa Israel iliweka pampu tano karibu na kambi ya wakimbizi ya Shati huko Gaza mwezi uliopita.

Maofisa hao wanaeleza siku chache zilizopita kuwa Marekani ilipewa taarifa kuhusu mpango huo wa kusababisha mafuriko huko Gaza, na kwamba hadi sasa Israel haijathibitisha kama itaendelea na mpango huo kwakuwa huenda inapima usalama wa mateka ambao bado wako Gaza.



Hali ya makazi ilivyo kwa wananchi huko Ukanda wa Gaza. **PICHA: MTANDAO**

### HOFU YAONGEZEKA

Licha ya mpango huo, hofu miongoni mwa Wapalestina imezidi kuongezeka baada ya Israel kuzidisha mashambulizi katika Ukanda wa Gaza, ikiwa ni pamoja na karibu na hospitali na kusini mwa eneo lililozingirwa ambapo operesheni ya ardhini inazidi.

Mkuu wa Baraza la Wakimbizi la Norway, anatoa angalizo kwamba mashambulizi ya kiholela ya Israel dhidi ya raia wa Palestina kusini mwa Gaza yamefikia kipimo kipya, jambo ambalo limezidi kuongeza hofu.

Shirika la Hilali Nyekundu la Palestina linasema lilipoteza mawasiliano na timu zake baada ya huduma za mawasiliano kukatika huko Gaza kutokana na mashambulizi ya Israel.

Aidha, Jeshi la Israel linaeleza kuwa limeizingira kambi ya wakimbizi ya Jabalia huko Gaza baada ya kuharibu kile ilichokiita miundombinu ya kigaidi, ikibainishwa kwamba kambi hiyo ni kubwa zaidi na ilikuwa ikilengwa na mashambulizi ya anga kwa muda na kusababisha mauaji ya watu.

Pia jeshi hilo linasema vikosi vya Israel vilishambulia malengo kadhaa ya kigaidi ya Hezbollah baada ya kuvuka kaskazini mwa Israeli kutoka Lebanon, ambayo yalianguka katika maeneo ya wazi.

Linabainisha kwamba ndege za kivita zililenga miundombinu ya kigaidi na vituo vya kijeshi vinavyotumiwa kuhifadhi silaha na magaidi.

### SAKATA LA WHO

Hata hivyo, baada ya kuzuka taarifa kwamba Jeshi la Israel limelitaka Shirika la Afya Duniani (WHO) kuondoa ghala la msaada wa matibabu kusini mwa Ukanda wa Gaza ndani ya saa 24, kama kiongozi wake alivyodai. Jeshi hilo limeibuka na kukanusha madai hayo.

Mkuu wa shirika hilo Tedros Ghebreyesus, kupitia mtandao wake wa X (zamani Twitter) anasema "WHO imepokea taarifa kutoka kwa Jeshi la Ulinzi la Israeli kuondoa vifaa vyetu kwenye ghala letu la matibabu lililoko kusini mwa Ukanda wa Gaza ndani ya saa 24, kwani operesheni za ardhini zitalifanya lisiweze kutumika".

"Tunatoa wito kwa Israeli kuondoa agizo hili na kuchukua hatua zote zinazowezekana kulinda raia na miundombinu ya kiraia, ikiwa ni pamoja na hospitali na vifaa vya kibinadamu," amesema Ghebreyesus.

Vile vile, Chombo cha Ulinzi cha Israeli kinachosimamia shughuli za kiraia katika maeneo ya Palestina (COGAT) kimejibu ujumbe huo kikikanusha kauli hiyo ya WHO.

"Ukweli ni kwamba hatukuomba kuhamisha maghala na tuliliweka hili wazi na kwa maandishi kwa maofisa husika wa Umoja wa Mataifa (UN). Tunatarajia ofisa wa umoja huo angalau kuwa sahihi katika maelezo yake," imesema COGAT.

Mkurugenzi wa Ofisi ya Kanda ya WHO katika eneo la Mediterania ya Mashariki, Ahmed Al-Mandhari, anasema shirika hilo linasikitishwa sana na kuanza tena kwa mapigano, ikiwa ni pamoja na mashambulizi makubwa ya mabomu huko Gaza.

Mwakilishi wa WHO huko Palestina, Richard Peeperkorn, anaeleza kwamba "hali inazidi kuwa mbaya zaidi kwa sasa. Kuna mashambulizi makali ya mabomu yanayoendelea pande zote, ikiwa ni pamoja na hapa katika maeneo ya kusini, Khan Younis na hata Rafah".

### MSISITIZO WA UN

Msemaji wa UN, Stephane Dujarric, anasema umoja huo unaendelea kuvisisitiza vikosi vya Israel kuepuka hatua zaidi zitakazozidisha hali ya janga la kibinadamu huko Gaza na kuwaepusha raia na mateso zaidi

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, anaelezea wasiwasi wake mkubwa kuhusu kuanza tena kwa mapigano kati ya Israel na Hamas, ikijumuisha ufyatuaji wa roketi wa Hamas kwa Israel na kuongezwa kwa mashambulizi ya anga na operesheni za kijeshi za ardhini za Israel katika eneo la kusini mwa Gaza.

Anasema wananchi, wafanyakazi wa afya na mashirika mengine, pamoja na miundombinu, ni lazima ilindwe wakati wote.

Huku akisisitiza pande zote kuheshimu wajibu wao chini ya sheria ya kimataifa ya kibinadamu na kusitisha mapigano.

### QATAR

Kiongozi wa Kidini wa Qatar Sheikh Tamim bin Hamad, ametoa karipio kali kwa Israel katika hotuba yake ufunguzi wa mkutano wa kilele wa Baraza la Ushirikiano wa Ghuba (GCC) mjini Doha, ikieleza kwamba mauaji yanayotekea huko Gaza ni sawa na ya kimbari.

"Vikosi vinavyokalia kwa mabavu vya Israel vimekiuka maadili yote ya kisiasa, kimaadili na kiutu. Ni aibu kwa jumuiya ya kimataifa kuruhusu uhalifu huu wa kutisha kuendelea kwa mauaji ya kimfumo na ya makusudi ya raia wasio na hatia. Haya ni mauaji ya kimbari yaliyofanywa na Israel," amesema Sheikh Hamad

Anasema kuwa Wapalestina wanapaswa kupongezwa kwa kushikilia msimamo wao wa haki na kutoa wito wa kusitishwa kwa mapigano kamili na ya kudumu.

### UFARANSA

Katika hatua nyingine Ufaransa imeweka kizuizi cha mali kwa, kiongozi wa Hamas huko Gaza, Yahya Sinwar, kutokana na amri iliyochapishwa katika jarida rasmi la nchi hiyo.

Mwezi uliopita, Ufaransa iliweka vikwazo katika ngazi ya kitaifa kwa makamanda wa kijeshi Mohammed Deif na naibu wake, Marwan Issa.

Wanadiplomasia wa Ufaransa wanasema wanafanya kazi na washirika kuweka vikwazo kwa wanachama wa Hamas na mtandao wa ufadhili wa kundi hilo katika ngazi ya Umoja wa Ulaya (EU).

***Chanzo mashirika ya kimataifa.***


**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
**Ofisi ya Rais**
**MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU

Wananchi wote mnatangaziwa kwamba Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) itauza kwa njia ya mnada wa hadhara Magari chakavu katika Mkoa wa Dar es Salaam na Mbeya katika vituo na tarehe kama ilivyooneshwa hapa chini:

| Na | AINA YA GARI ZITAKAZOUZWA | IDADI | KITUO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Landrover Defender 110 | 17 | TASAF OFFICE DSM | 21/12/2023 |
| | Land rover 90 | 13 | | |
| | Suzuki Garnd | 2 | | |
| | Nissan Patrol | 1 | | |
| 2 | Landrover Defender 110 | 18 | VETA KEKO DSM | 22/12/2023 |
| | Landrover 90 | 17 | | |
| | Suzuki Grand Vitara | 4 | | |
| 3 | Landrover Defender 110 | 1 | ILEJE MBEYA- OFISI YA HALMASHAURI | 23/12/2023 |
| | **JUMLA** | **73** | | |

**MASHARTI YA MNADA**

i. Gari itauzwa kama ilivyo na mahali ilipo
ii. Mnunuzi atalazimika kulipa papo hapo amana (Deposit) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari atakayonunua, na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa gari husika na amana iliyolipwa haitarudishwa.
iii. Mtu yoyote atakaetamka bei ya juu kisha akashindwa kulipa atachukuliwa kuwa ni mwenye kutaka kuvuruga mnada na hivyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake kwa mujibu wa Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
iv. Mnunuzi atatakiwa kuondoa gari atakayonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia tarehe ya kukamilisha malipo.
v. Ruhusa ya kuangalia magari yanayokusudiwa kuuzwa itatolewa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya mnada husika
vi. Mnada utaanza saa nne kamili (04:00) asubuhi katika kila kituo.

**Kaimu Mkurugenzi Mtendaji**
**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii – TASAF**
**Barabara ya Jakaya Mrisho Kikwete**
**S. L. P 2719 Dodoma,Tanzania**
**Simu: 255 026 2963866**
**Nukushi: 255 026 2963871**
**Barua pepe: info@tasaf.go.tz**
**Tofuti: www.tasaf.go.tz**

177437

# RAYVANNY ANOGESHA UZINDUZI KAMPENI YA VUNA DEILE YA ITV

**Mwandishi Wetu**

MWANAMUZIKI, Raymond Shaban maarufu Rayvanny, amekonga nyoyo za mashabiki juzi jioni wakati akizindua Kampeni ya Vuna Deile, inayofanyika kote nchini ikilenga kutoa zawadi mbalimbali kwa Watanzania kipindi hiki cha sikukuu za mwisho wa mwaka na mwakani.

**Miongoni mwa zawadi hizo ni pesa taslimu Sh. milioni 10 na gari moja mpya aina ya IST kila siku kuanzia leo.**

Akizungumza katika shoo ya kutambulisha kampeni hiyo, Rayvanny, alisema huo ni mwanzo wa kufanya vitu vingine vingi vizuri.

"Leo (juzi jioni) ilikuwa ni shoo ya kutambulisha kampeni hii, mashabiki wangu na wananchi wakae mkao wa kula, mambo mengi mazuri yanakuja katika kampeni hii ya Vuna Deile," alisema Rayvanny.

Katika shoo yake, iliyofanyika kwenye viwanja vya ITV, Rayvanny aliimba nyimbo kadhaa zilizokonga nyoyo za mashabiki kama ule wa 'Forever, Nakupenda' na nyingine nyingi.

"Kama nilivyosema mambo mazuri yanakuja kwenye Vuna Deile, mashabiki na Watanzania wajiandae, wapo watakaoshinda ndinga, wengine mkwanja kila siku," alisema.

Akizungumzia kampeni hiyo, Naseem Allan, ambaye ni mratibu alisema inatoa nafasi kwa kila Mtanzania kucheza.

"Kipindi hiki cha sikukuu za mwisho wa mwaka na hata mwakani mambo yatakuwa ni mazuri kwa wachezaji wetu, tumetoa fursa hii ili kuwapa mzuka wa kusherehekea sikukuu vema wakiwa na pesa na wengine kushinda magari," alisema.

Alisema kuanzia leo Jumatano, washindi 10, kila mmoja ataondoka na kitita cha shilingi milioni moja.

"Pia kuna zawadi ya gari IST mpya kila siku kwa mshindi mmoja, hii inakuwa imelipiwa kila kitu, unachohitaji ni leseni tu ili kuanza kuiendesha," alisema Naseem na kufafanua kwamba kampeni hiyo ni endelevu hadi mwakani na kila siku inatoa washindi 10 wa milioni moja kila mmoja, na mshindi mmoja wa gari.

"Leo tumezindua kampeni hii ambayo unacheza kwa buku (Sh. 1000) na kuingia kwenye kinyang'anyiro cha kushinda," alisema.

Alisema kampeni hii inafanywa kwa ushirikiano na ITV ambako itaonyeshwa mubashara kila siku kuanzia saa 12 jioni.

"Zawadi ni nyingi na kila Mtanzania anaweza kucheza kwa kuzingatia vigezo na masharti, itafanyika kila siku na hii inaonyesha ni namna gani tunavyokwenda kuumaliza mwaka na kuanza mwingine vizuri," alisema.

"Kifupi unapanda buku, unavuna ndinga na milioni 10 kwa watu 10 kila siku wanagawana," alisema.

Kampeni hiyo yenye kaulimbiu ya panda, vuna, utimize ndoto inachezwa kwa Namba ya Kampuni 664455 na kuweka kumbukumbu namba ambayo ni namba ya simu yako kwa Sh. 1000 unaingia kwenye kinyang'anyiro.



Msanii Rayvanny akitumbuiza wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya Vuna Deile inayoendeswa na Kituo cha Televisheni cha ITV. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Ihefu FC yatimiza miezi miwili bila ushindi

**Na Adam Fungamwango**

SULUHU dhidi ya Tanzania Prisons juzi kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali mkoani Mbeya, imeifanya timu ya Ihefu FC kufikisha miezi miwili kamili bila kupata ushindi wowote kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Mara ya mwisho kushinda mechi yake ya ligi, ilikuwa ni Oktoba 4, mwaka huu, kwenye uwanja wake huo wa nyumbani, ikiifunga Yanga mabao 2-1, lakini tangu wakati huo haijapata tena ushindi wowote.

Tangu ilipoifunga Yanga, Ihefu imecheza mechi nane, ikipoteza michezo minne na kutoka sare minne pia.

Kocha Moses Basena aliyeiongoza timu hiyo kwenye michezo saba amelaumu wachezaji wake kuwa hawakutumia nafasi walizotengeneza.

"Si rahisi kushinda kama unatengeneza nafasi halafu hazitumii, ili ushinde inabidi utumie nafasi, huwa tunacheza vizuri sana, lakini kinachotugharimu ni kuweka mpira ndani ya wavu," alisema kocha huyo wa zamani wa Simba.

Naye kocha mpya wa Prisons aliyeichukua timu hiyo badala ya Fred Felix Minziro, Ahmad Ally, amewapongeza vijana wake kwa kuweza kutwaa pointi moja ugenini.

Alisema kwa sasa kikosi chake kinacheza vema na kutengeneza nafasi, kilichobaki sasa ni kutulia kwa kuweka mipira kwenye kamba.

## KMKM yarejesha makali Ligi Kuu Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya KMKM SC imerudi katika mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kushinda michezo miwili mfululizo .

KMKM juzi iliibuka na ushindi katika mchezo wake wa 14 baada ya kuwafunga Wanajeshi wa Kipanga bao 1-0 mechi ikipigwa katika Uwanja wa Mau A majira ya saa kumi alasiri.

Kwa matokeo hayo KMKM SC imefikisha alama 26 ikiwa nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo huku kinara ikiwa ni JKU SC na alama zake 32, ikifuatiwa na Zimamoto SC yenye alama 29.

Akizungumza na Nipashe Kocha Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu (pichani chini), alisema wanaendelea kuimarika kidogo kidogo kurejea katika mstari wake wa kupata matokeo mazuri.

Alisema licha ya kupata ushindi wa michezo miwili mfululizo, lakini bado timu hiyo haichezi kama ilivyozoeleka, hivyo wanahitaji kuhakikisha wachezaji wanaonesha kandanda safi kama msimu uliopita.

Alisema kwa kuanzia lazima benchi la ufundi lihakikishe linatoa hamasa kubwa kwa wachezaji hasa kabla na baada ya mchezo.

"Bado timu haijajishika vizuri, katika mpira ni kawaida timu kukumbwa na hali kama hii ya kupoteza michezo mara kwa mara, jambo linalosababisha wachezaji kuvunjika moyo na kupoteza matumaini mapema, hivyo lazima tuwarejeshe katika hali yao ya kawaida," alisema.

Aidha, alisema katika mchezo wao huo dhidi ya Maafande wa Kipanga FC kipindi cha kwanza hawakucheza vizuri, lakini cha pili walisawazisha makosa yao na kurejea mchezoni na kufanikiwa kupata bao.

Hata hivyo, alisema hivi sasa wanajiandaa na mchezo wao wa mwisho wa 15 wa kukamilisha mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya Mlandege FC.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### RAMSDALE NAYE AFIKIRIWA

GOLIKIPA wa Arsenal, Aaron Ramsdale pia anafikiriwa kuhamia Newcastle United, lakin klabu hiyo inasita kutoa kitita kinachotakiwa na Arsenal cha pauni milioni 50 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Talksport)***

#### GUIRASSY AWINDWA

KLABU za Newcastle na Manchester United zinawania kumnunua mshambuliaji wa Guinea, Serhou Guirassy mwenye umri wa miaka 27 kutoka Stuttgart Januari. ***(Football Insider)***

#### NKETIAH KUPELEKWA SOKONI

ARSENAL iko tayari kusikiliza ofa kwa mshambuliaji wake, Eddie Nketiah mwenye umri wa miaka 24, wakati wa dirisha la Januari. ***(Football Transfers)***

#### VARANE KUBAKI UNITED

MLINZI wa zamani wa Ufaransa, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 30, ameelezea nia yake ya kubakia Manchester United baada ya dirisha la usajili la Januari. ***(Manchester Evening News)***

#### MAIGNAN KUNG'OLEWA

KLABU za Manchester United, Arsenal na Chelsea zinamfuatilia golikipa wa Ufaransa, Mike Maignan mwenye umri wa miaka 28, huku akikwama kusaini mkataba mpya na AC Milan. ***(Footmercato)***

#### TEL AWANIWA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich inakabiliwa na kibarua cha kumbakisha mshambuliaji Mfaransa, Mathys Tel mwenye umri wa miaka 18, huku klabu kadhaa za Ligi Kuu England zikimtaka. ***(Bild)***

#### MATETA KUONDOKA PALACE

MCHEZAJI Jean-Philippe Mateta anataka kuondoka Crystal Palace Januari na Eintracht Frankfurt inaweza kumpa mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 26 ruhusa ya kuondoka. ***(The Athletic)***

#### PHILLIPS AWANIWA JANUARI

KLABU ya Newcastle United inatazamiwa kumsajili kiungo wa kati wa Manchester City na Timu ya Taifa ya England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 28, katika dirisha la Januari. ***(Rudy Galetti)***

#### NYOTA ARGENTINA WASAKWA

CHELSEA na Manchester City zimeonesha nia ya kutaka kumnunua kiungo wa kati wa River Plate, Claudio Echeverri mwenye umri wa miaka 17, mshambuliaji Agustin Ruberto (16) na winga Ian Subiabre, ambao walionesha kiwango cha juu wakati wakiichezea Argentina Kombe la Dunia la chini ya umri wa miaka 17. ***(90Min)***

#### CASHIN NA WEST HAM

WEST Ham, Burnley na Sheffield United zinatazamiwa kunasa saini ya beki wa Derby, Eiran Cashin, 22. ***(TeamTalk).***

#### FOREST NA VIKWAZO

KLABU ya Nottingham Forest inaweza kukabiliwa na vikwazo vya uhamisho wa Januari juu ya malipo ya ada ya kuchelewa inayodaiwa na mawakala. ***(The Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# DE GEA NJIA NYEUPE KUITUMIKIA NEWCASTLE

**NEWCASTLE,** England

●●● Licha ya kuhusishwa na kipa wa Arsenal, Ramsdale, sasa inamwona...

KLABU ya Newcastle United imepewa nafasi ya kumsajili golikipa David de Gea kwa uhamisho wa bure, kwa mujibu wa 90min.

**'The Magpies' wamepata pigo kubwa katika idara ya makipa baada ya mlinda mlango, Nick Pope, kuteguka bega wakati wa ushindi wao wa bao 1-0 nyumbani dhidi ya Manchester United Jumamosi usiku.**

90min ilripoti mapema Jumatatu kwamba Newcastle wamesema Pope atarudi dimbani Aprili mwakani, huku uamuzi wa kama atafanyiwa upasuaji au la utaamuliwa wiki hii.

Licha ya kuhusishwa na kipa wa Arsenal, Aaron Ramsdale, Newcastle inamwona De Gea kama mtu sahihi kwao.

De Gea hajaharakishwa kufanya maamuzi kuhusu mustakabali wake baada ya kuondoka Man Utd mwishoni mwa mkataba wake msimu huu wa majira ya joto, akipuuza ofa kutoka kwa Al Nassr ya Cristiano Ronaldo kwenye Ligi Kuu ya Saudi Arabia.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, pia hivi karibuni ameibuka kama chaguo kwa Klabu ya Inter Miami ya Marekani ambayo anaichezea Lionel Messi.

Newcastle inaogopa kutumia fedha nyingi kumnunua golikipa mpya Januari kwani itakuwa imekiuka kanuni za haki sawa za kifedha kwenye usajili.

Kwa sababu sawa na hizo, wanatumaini Manchester City itakubali kumtoa kwa mkopo kiungo Kalvin Phillips, lakini hii itachukua nafasi ya pili kati ya nafasi zao mbili za mkopo wa ndani - nyingine imejazwa na Lewis Hall wa Chelsea.

Kwa hiyo, uhamisho wa mchezaji huru kama De Gea ungewezekana zaidi kwa Newcastle, ambao hawatalazimika kugeukia soko la mkopo kutafuta suluhisho la muda la golikipa na badala yake wanaweza kumsajili raia huyo wa Hispania kwa mkataba wa muda mfupi.

# WACHEZAJI MAN UNITED WAINGIA BIFU NA TEN HAG



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, anapambana kuwaweka wachezaji wake muhimu upande wake baada ya kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Newcastle United, vyanzo vimeiambia ESPN.

Kundi ndani ya kikosi cha kwanza linazidi kukata tamaa baada ya kufungwa mara ya 10 msimu huu kwenye Uwanja wa St James' Park Jumamosi.

Wachezaji kadhaa wamesalia nyuma ya Ten Hag na benchi la ufundi, lakini kuna wasiwasi ndani ya klabu kwamba morali ndani ya vyumba vya kubadilishia nguo itapungua zaidi kama hakutakuwa na mabadiliko ya kiwango cha timu.

Man United inakabiliwa na mechi muhimu dhidi ya Chelsea, Bayern Munich na Liverpool katika wiki mbili zijazo.

Miongoni mwa mambo yanayozungumziwa pembeni na baadhi ya wachezaji ni pamoja kuchoshwa na mazoezi makali ya Ten Hag tangu ziara ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani, na kile kinachochukuliwa kuwa mbinu za kivita ambazo zimeiacha wazi timu hiyo, hasa wakati wa sare ya 3-3 dhidi ya Galatasaray na kufungwa na Newcastle.

Kwa mujibu wa ESPN, Ten Hag amejaribu kupoza hali ya hewa ndani ya kikosi hicho kwa kuwaunga mkono wachezaji wake hadharani licha ya kufanya vibaya.

Alikataa kumkosoa mlinda mlango Andre Onana kwa makosa yake dhidi ya Galatasaray na pia alitaka Marcus Rashford aungwe mkono licha ya uchezaji wake duni dhidi ya Newcastle.

Kuna hisia zinazoshikiliwa na baadhi ya wafanyakazi kuwa baadhi ya wachezaji hawaitikii vema wanapokosolewa, hasa maoni yanayotolewa hadharani. Imeelezwa kuwa Lisandro Martinez ambaye ni mfuasi mkuu wa Ten Hag, amerejea katika kundi la kwanza licha ya kuwa nje ya uwanja kutokana na majeraha.

Martinez anapata nafuu baada ya kufanyiwa operesheni ya pili ya kurekebisha tatizo la mguu na hatakiwi kurejea uwanjani hadi baada ya Krismasi, lakini beki huyo wa Argentina amepigwa picha akitazama mazoezi huko Carrington.

# Arteta ataka Ramsdale abaki Arsenal




**LONDON,** England

MIKEL Arteta amesisitiza kwamba anataka Aaron Ramsdale kubakia Arsenal licha ya kuwapo kwa uvumi kuwa anaondoka katika klabu hiyo Januari.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ameanza mchezo mmoja pekee wa Ligi Kuu England tangu Septemba 3, mwaka huu, huku David Raya aliyesajiliwa kwa mkopo majira ya joto akichukua nafasi yake kama namba moja wa 'Washikabunduki' hao.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Ramsdale inavutiwa na klabu kadhaa za England zikiwamo Chelsea na Wolverhampton Wanderers, wakati Newcastle United iko sokoni kutafuta golikipa baada ya kuumia kwa Nick Pope ambaye atakuwa nje ya dimba kwa kipindi cha miezi minne.

Lakini Arteta alisema: "Namtaka Aaron pamoja nasi. Nina furaha sana kuwa na makipa wawili wazuri sana na Aaron anabaki nasi."

Kocha wa England, Gareth Southgate ameonya Ramsdale kuwa nafasi yake kwenye kikosi cha timu ya taifa inaweza kuwa hatarini ikiwa hatapata muda zaidi wa kucheza, lakini Arteta alisisitiza kuwa "hatarajii" hilo kuwa suala kubwa.

"Je, nimezungumza naye kuhusu hilo? Ndiyo," alieleza Arteta. "Yuko tayari kucheza. Kama mchezaji yeyote, anataka kuichezea Arsenal. Hilo ndilo analotaka kufanya. Kisha mengine ni matokeo.

"Na vile vile kwa England si kama ameanza mechi nyingi, kwa hiyo tunatumaini tunaweza kumsaidia kuwa bora hapa ili aweze kucheza England.

"Tunataka awe bora zaidi, kwa hiyo tunataka kuongeza kile tulichonacho. Hiyo ndiyo nia tuliyo nayo."

# Haaland apona, FA yaishitaki Man City

**LONDON,** England

ERLING Haaland ameepuka adhabu kutoka Chama cha Soka England kwa kukosoa uamuzi wa mwamuzi, Simon Hooper, kusimamisha mchezo wakati Manchester City ilipotoka sare ya mabo 3-3 dhidi ya Tottenham Jumapili, lakini mabingwa hao wa Ligi Kuu England wameshtakiwa kwa kushindwa kudhibiti mienendo ya wachezaji wao.

Mshambuliaji wa City, Haaland alikosoa uamuzi wa Hooper kupitia kwenye ukurasa wake wa X (zamani twitter) kwa kutomruhusu Jack Grealish kufunga katika dakika ya nne ya muda wa mapumziko mwishoni mwa mchezo.

Vyanzo vya FA vimeiambia ESPN, kwamba chapisho la Haaland halikukiuka sheria kuhusiana na kanuni zinazohusu maoni ya vyombo vya habari.

Haaland, mfungaji kinara wa Ligi Kuu hadi sasa msimu huu, pia ameepuka kulaumiwa kwa kumkabili Hooper uwanjani kwa hasira kufuatia uamuzi wa kupuliza kipenga Grealish alipopokea mpira.

Tukio hilo lililowahusisha Haaland na Hooper ni kiini cha City kushtakiwa kwa ukiukaji wa Kanuni ya FA E20.1 kuhusiana na mienendo ya wachezaji wao.

Haaland aliongoza kundi la wachezaji, akiwamo Ruben Dias na Mateo Kovacic, ambao walimzunguka Hooper kupinga uamuzi huo.

Katika taarifa, FA ilisema: "Manchester City imeshtakiwa kwa ukiukaji wa Kanuni ya FA E20.1 baada ya wachezaji wao kumzingira afisa wa mechi wakati wa mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Tottenham Hotspur Jumapili, Desemba 2023.



# Kipenga FA Cup Z'bar chapulizwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MICHUANO ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanziba (ZFF) maarufu FA Cup, kwa hatua ya awali inatarajiwa kuanza kutimua vumbi Desemba 24, mwaka huu kwa Unguja na Pemba, imeelezwa.

Michuano hiyo inachezwa kwa Kanda mbili kwa Unguja na Pemba ambapo bingwa wa Kanda ya Unguja atakutana na bingwa wa Kanda ya Pemba ili kupata timu itakayo iwakilisha Zanzibar katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Michuano hiyo kwa ngazi ya awali kwa upande wa Unguja itakuwa na jumla ya timu 40 kutoka katika klabu za Ligi Daraja la Kwanza na mikoa mitatu ya Unguja.

Kwa upande wa timu za Daraja la Kwanza Kanda itazijumuisha timu 20 na timu 10 zitatoka katika Mkoa wa Mjini Magharibi, Mkoa wa Kaskazini Unguja timu tano na Kusini Unguja timu tano.

Kwa upande wa Pemba kutakuwa na jumla ya timu 24, timu 18 kutoka Ligi Daraja la Kwanza kanda hiyo na timu sita kutoka mikoa miwili ya Kisiwani Pemba ambayo ni Kaskazini na Kusini.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Ali Bakari 'Cheupe', alisema ratiba ya michuano hiyo inatarajiwa kutoka leo ili timu ziendelee na maandalizi ya kuwania kombe hilo.

Alisema wanaendelea kutafuta wadhamini ili kuleta ushindani zaidi katika hatua ya mwanzo mpaka mwisho wa michuano hii ya FA.

"Michuano hii mara zote huwa na mvuto mkubwa hasa timu za madaraja ya chini kanda na mikoa huonesha upinzani wa hali ya juu, hivyo tunahangaika kutafuta wadhamini ili klabu zipate fedha za udhamini ambazo zinatachangia kuleta ushindani mkubwa zaidi," alisema Cheupe.

Hata hivyo, alizitaka klabu zinazoshiriki michuano hiyo kuzingatia kanuni, lakini pia kushiriki kwa malengo kama ilivyokuwa kwa timu za Ligi Kuu.

# DABO ASUGUA KICHWA RATIBA NGUMU DESEMBA KWA AZAM

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Youssouph Dabo, amekiri ana kibarua kigumu Desemba hii katika kuhakikisha timu yake inavuna pointi za kutosha katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la Shirikisho la Azam (FA Cup).

Azam FC katika mwezi huu wa kufungia mwaka wana michezo sita, mitano ya Ligi Kuu na mmoja wa FA dhidi ya Alliance FC utakaopigwa kati ya Desemba 15 hadi 17, mwaka huu, katika Uwanja wa Azam Complex, uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

**Kibarua cha kwanza kwa Dabo atakuwa nyumbani dhidi ya KMC FC ambayo ipo nafasi ya nne huku ikinolewa na kocha aliyewahi kukinoa kikosi cha Azam FC, Abdihamid Moalin, ambaye amekuwa na matokeo mazuri kwa timu hiyo.**

Siku chache baadaye Azam FC watakutana na JKT Tanzania, Uwanja wa Azam, uliopo Chamazi, halafu watakuwa na mchezo wa FA dhidi ya Alliance FC kuanzia Desemba 15 -17, baadaye itakuwa na kibarua kigumu cha michezo mitatu ya ligi dhidi ya Kagera Sugar Desemba 21, Uwanja wa Kaitaba na kisha dhidi ya Geita Gold ambayo bado haijapangwa tarehe utakaochezwa Azam Complex na mwingine watalazimika kufunga safari kuwafuata Tabora United.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Azam FC, Dabo alisema malengo yao ni kuona wanashinda na kuvuna alama zote katika michezo mitano ya ligi na mmoja wa FA.

Alisema anatambua hakuna mechi rahisi kulingana na wapinzani watakaokutana nao ikiwamo mechi yao ya hivi karibuni dhidi ya KMC FC ambayo anaamini itakuwa na ushindani mkubwa kutokana na benchi la ufundi imara la wapinzani wao.

"Malengo yetu ni kuhakikisha tunashinda michezo iliyosalia ya mzunguko wa kwanza pamoja na mechi yetu ya FA, kwa sasa tunaangalia mechi iliyopo mbele yetu dhidi ya KMC FC, tunahitaji kupata ushindi na kuvuna alama tatu," alisema Dabo.




Waziri wa Maliasili na Utalii wa Tanzania, Angellah Kairuki (katikati), akikabidhi zawadi ya ukumbusho kwa wachezaji maarufu wa mchezo wa tenisi John na Patrick McEnroe (kushoto) katika hafla ya chakula cha jioni iliyofanyika jijini Arusha juzi ikiwa pia ni uzinduzi wa mashindano ya tenisi yatakayofanyika Desemba 8 mkoani Mara na kudhaminiwa na Shirika la ndege la KLM. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Yanga yaitaka rekodi mpya

INATOKA UKURASA 24

wa Yanga, Ali Kamwe, alisema wachezaji wote wako na morali kubwa kwenda kutafuta furaha za mashabiki wa Yanga na kufikia malengo yao.

Alisema katika kikosi hicho hatakuwapo Lomalisa ambaye yuko kwenye uchunguzi baada ya kuumia katika mechi iliyopita dhidi ya Al Ahly na nafasi yake kuchukuliwa na Kibabage .

"Ni kweli tutamkosa Lomalisa, lakini hatuna presha kutokuwapo kwake kwa sababu yupo Kibabage ni mzuri na atafanya kazi yake ipasavyo, tumeshamwona katika michezo iliyopita jinsi anavyocheza.

Presha ya mchezo ni lazima kwa sababu kila dakila 90 zinapokamilika basi mahesabu yanabadilika, mchezo ni mgumu tunaenda kucheza ugenini na ukizingatia Medeama wamemfunga aliyetufunga CR Belouizdad, hivyo watakuwa wanajiamini.

"Watambue tu kuwa Yanga si mpinzani mwepesi, tunahitaji kutafuta matokeo mazuri ikiwamo ushindi ili hesabu zetu ziweze kukamilika," alisema Kamwe.

Aliongeza kuwa wanatambua katika rekodi dhidi ya Belouizdad walipoteza ugenini mabao 3-1 mwaka 2016 na katika mchezo wa marudiano kutoka sare ya bao 1-1 nyumbani, hivyo wanasahau hayo na wanaenda kutafuta ushindi ili kukamilisha hesabu zao.

"Tunajua historia lakini hesabu zetu ni jinsi ya kufikia malengo yetu, tumepoteza mechi moja, kutoka sare moja, sasa tunahitaji alama tatu za mchezo iliyopo mbele yetu tukianza dhidi ya Medeama," alisema.

# Benchikha aanika gonjwa Simba

INATOKA UKURASA 24

"Mungu akitujalia kufika siku ya Jumatano (leo) kama tunavyotegemea, moja kwa moja tutafanya mazoezi, Alhamisi tutaendelea na Ijumaa pia, kabla ya kucheza mechi yetu Jumamosi kwa ajili ya kupigania pointi tatu dhidi ya timu hiyo.

Wachezaji ni 23, na watakaobaki ni wale ambao hawatokuwa kwenye mipango ya kocha, watabaki kwa sababu za kiufundi na si za kimajeraha," alisema.

Ahmed pia amewasifu makocha hao kwa kuonekana kurudisha kiwango cha utimamu wa mwili wachezaji wa timu hiyo.

"Kwanza nimeona utimamu wa mwili umeongezeka sana ni moja kati ya vitu ambavyo vimetusumbua kwa muda mrefu, nadhani tumpe pongezi zake huku mwalimu mpya Benchikha wa viungo Kamal, kwa siku hizi zilizobaki, wamesema ndiyo eneo linalofanyiwa sana kazi, nadhani huko mbele timu itakuwa tishio," alisema.

Michezo
Jumatano Desemba 6, 2023
Nipashe



Wachezaji United waingia bifu na Ten Hag UKURASA 22

# Yanga yaitaka rekodi mpya kwa Medeama CAF

**Na Saada Akida**

● ● ● Morali ya wachezaji juu, Gamondi apania kuishangaza kwa...

KATIKA kuhakikisha anapata pointi tatu za kwanza hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika na dhidi ya Medeama SC, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, anatarajia kuwachanganya wapinzani wao hao, kwa kufanya mabadiliko madogo ya kikosi chake kuelekea mechi yao hiyo ya tatu kwenye hatua hiyo.

Yanga ambayo imeshacheza michezo miwili ya hatua hiyo ya makundi, ikianzia ugenini nchini Algeria ambapo ilipoteza kwa mabao 3-0 dhidi ya CR Belouizdad kabla ya kurejea nyumbani katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na kulazimisha sare ya bao 1-1 dhidi ya Al Ahly ya Misri, Ijumaa itashuka katika Uwanja wa Baba Yara Sports (pia ukijulikana kama Uwanja wa Michezo wa Kumasi), kusaka alama tatu za kwanza.

Kama itapata ushindi, kwanza itaandika rekodi yao dhidi ya Medeama kwa kuifunga mara ya kwanza katika historia yake tena nyumbani, lakini huo utakuwa ushindi wao wa kwanza kwenye hatua hiyo msimu huu.

**Mara ya kwanza timu hizo kukutana katika michuano hiyo ilikuwa mwaka 2016, Yanga ikikubali kichapo cha mabao 3-1 ugenini na mechi ya marudiano kutoka sare ya bao 1-1 hapa nchini.**

Mabadiliko ambayo Gamondi anatarajia kuyafanya ni katika safu ya ulinzi baada ya beki Joyce Lomalisa kutoongozana na timu kutokana na kuwa majeruhi baada ya kuumia kwenye mchezo uliopita dhidi ya Al Ahly ya Misri na nafasi yake kuchukuliwa na Nickson Kibabage.

Tayari Kikosi cha Yanga kilionduka tangu jana alfajiri kuelekea Ghana kwa ajili ya kusaka alama tatu muhimu zitakazoweza kuwatoa mkiani mwa Kundi D, lakini kutegemeana na matokeo ya mchezo kati ya Al Ahly dhidi ya Belouizdad.

Al Ahly inaongoza msimamo wa Kundi D ikiwa na pointi nne ikifuatiwa na Medeama na Belouizdad ambazo kila moja ina alama tatu huku Yanga ikiwa na moja, hivyo kama itashinda na miamba hiyo ya Misri kuwachapa Waalgeria hao, itapanda hadi nafasi ya pili.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari na Mawasiliano

INAENDELEA UKURASA 23



Gamondi



Wachezaji wa Simba wakiwa Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere jana tayari kwa safari ya Morocco kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad Jumamosi wiki hii. **PICHA: SIMBA**

## Benchikha aanika gonjwa la Simba

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha wachezaji 23 wa Klabu ya Simba, kimeondoka jana saa tisa alasiri na ndege ya Shirika la Ndege la Qatar kwenda Casablanca nchini Morocco kwa ajili ya mechi ya raundi ya tatu ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kundi B dhidi ya Wydad Casablanca utakaochezwa Jumamosi ijayo, huku Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha akiweka wazi kuwa amekuta wachezaji hawana utimamu wa mwili.

Kikosi hicho kilitarajiwa kuchukua usafiri mwingine wa aina hiyo kitakapotua jijini Casablanca kuelekea Marrakech na kuanza moja kwa moja mazoezi leo kwa ajili ya kujiandaa na mechi hiyo.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, kabla ya safari hiyo jana amebainisha kuwa kazi kubwa alinayo, pamoja na kuitengeneza kuifundi kwa ajili ya kukabiliana na Wydad Casablanca, lakini pia ni kupandisha kiwango cha utimamu wa mwili ambacho kilikuwa chini mno, katika namna ambayo imemshangaza hata yeye mwenyewe.

"Wachezaji hawakuwa na utimamu wa mwili, yaani ilikuwa chini ya kiwango na ndiyo eneo ambalo nimewekeza nguvu kweli kweli, kiufundi Simba ina wachezaji wazuri sana, levo ya utimamu wa mwili ndiyo inawasumbua, na nimemwachia kazi mwalimu mwenzangu Kamal Boujdjenane anaifanya kazi hiyo," alisema kocha huyo raia wa Algeria aliyechukua nafasi ya Roberto Oliveira.

Alisema anadhani ndiyo sababu inaonekana kama baadhi ya wachezaji wameshuka viwango, au wana umri mkubwa unaowafanya washindwe kukabiliana na mikikimikiki.

"Nadhani ndiyo ilionekana kama wachezaji wanaonekana kama viwango vyao vimefikia ukingoni, lakini kwa sasa inaanza kuongezeka na itaongezeka zaidi, kwa sasa tunahitaji angalau asilimia 50 tu ya ufiti wa wachezaji iweze kuwa kwenye ushindani unaotakiwa," alisisitiza kocha huyo.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo alisema timu iliondoka na wachezaji 23 tu na iliyowaacha ni kwa sababu za kiufundi na si majeruhi.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >